# *MUNGU HUTIMIZA NENO LAKE*

[Ndugu Neville anasema, “Mungu akubariki, Ndugu Branham.”—Mh.] Niombeeni. [“Amina.”]

2 Habari za asubuhi, marafiki. Ni majaliwa kuwa hapa asubuhi ya leo, katika ibada ya Bwana, na kuhisi makaribisho haya ya ajabu na ushirika. Ina maana kubwa kwa moyo wa msafiri, kuihisi roho hiyo ya makaribisho. Mnajua, inakujia tu, na kuna jambo fulani tu, ambalo halichukui mahali pake. Na kurudi maskanini tena, na, pia, katika ibada ya Bwana wetu mbarikiwa.

3 Na sasa tuna ibada ya kuwekwa wakfu watoto, lakini nafikiri tutaifikia tu hiyo katika dakika chache.

4 Tunakaribia Pasaka. Nadhani inakuja yapata tarehe ishirini na moja. Nami nilikuwa nataka kuja hapa mapema, kuwaona wazee na Ndugu Neville. Basi yapata . . . mimi . . . Labda lingekuwa jambo jema kama tungekuwa na mkutano mdogo hapa, kabla tu ya i—ibada ya Pasaka. Labda tuanze, tuseme, Jumatano na kuendelea hadi Jumapili, na kumalizia na ibada ya Ubatizo kwenye Jumapili ya Pasaka. Na kuwa na ninii kidogo . . . mkutano, kujumuika. Hii ni maskani ndogo nilimolelewa. Ndilo kanisa langu la kwanza na la pekee. Nami ningependa kurudi kwa ajili ya likizo hizi, na—na kumwabudu Bwana pamoja na nyinyi nyote. Nyote mngependelea hilo, mnafikiri lingekuwa tu ni mapenzi ya Bwana? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Naam. Vema, Bwana akipenda, tutaanza Jumatano, kabla ya Pasaka siku ya Jumapili.

5 Pia ningependa kusema kwamba labda tungemwuliza mweka hazina, au mdhamini na wao, kama wangeweka tangazo kidogo hapa gazetini mahali fulani. Na kuwaambia watoto kwamba tuko hapa kuabudu, nasi tungependa kuwa na ushirika pamoja nao wote. Maskini, kidogo kama kuja nyumbani, na kujiweka tayari . . .

6 Labda Bwana atatupatia ufufuo wa—wa—sehemu kubwa ya Roho Wake, akiendelea kwa ajili ya Pasaka hii ijayo. Ni—ni ninii . . . kama majira ya kupukutika na ya kuchipua. Nafikiri majira ya kuchipua ni wakati wa kupendeza, wakati kila kitu kinapoanza kuchukua umbo jipya na maisha mapya, na hutukumbusha ufufuo. Pasaka huja wakati unaofaa sana, kwenye majira ya kuchipua. Tukitambua, Neno la Mungu daima huendana moja kwa moja na maumbile Yake, na kadhalika. Kwa hiyo sisi ni . . .

7 Bwana akipenda, sasa, tutaanzisha hili. Na—na iwapo wataweka tangazo dogo, nilisema, gazetini. Na msilifanye la madoido. Waambie tu jamaa kwamba tunataka kumwabudu

Bwana pamoja. Nasi tungependa tu, wote wale ambao wangetaka kuja, kushiriki pamoja nasi, kidogo. Tutafurahia wakija, makanisa yote.

8 Basi wewe piga simu na kuwaambia jirani zako kuhusu hilo. Na uwaambie kwamba tunaenda tu kuzungumza kumhusu Bwana, na—na sote tuabudu tu pamoja.

9 Ningependa kuchukua hatua, kama itapendeza watu, na kuwa sawa machoni pa Mungu, na sawa na hao watatu, ningetaka hao Watatu wa Neville watusaidie kwenye wakati huo. Si mngefanya hivyo nyinyi nyote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni kweli. Kwa hivyo basi tutahakikisha kwamba tutashughulikiwa, kwa njia hii, ikiwa Bwana ataona kuwa inafaa kwetu kufanya hivyo. Kwa hiyo tunawaalika waimbaji wengine kutoka makanisa mbalimbali, waje na—na watusaidie tunapoendelea. Waimbaji kutoka kanisani mwako, tutafurahia kuwa nao. Mwone Ndugu Neville, labda usiku unaotangulia, na uweze kuwaweka kwenye ratiba, ili waweze kutuimbia.

10 Tunapenda uimbaji mzuri. Ningetaka tu kuwa na wakati mzuri wa kurudi nyumbani, wa mtindo wa kale, ambapo tunajumuika tu pamoja. Na mwite Angie. Wapi . . . Je, Dada Angie yuko hapa asubuhi ya leo? Mwite, ili yeye na Dada Gertie waweze kutuimbia *Wakati wa Kurudi Nyumbani* mara moja, na *Endelea Kushikilia*. Na huo ungeonekana kama mwanzo wa uamsho tena, Dada Gertie. Mambo mengi sana yamefanyika tangu tulipokuwa tukiimba huo hapa.

11 Nilikuwa na siku ya kuzaliwa jana, nami ni—ninajua mimi si kijana tena. Nikasema, "Nimepita miaka ishirini na minne sasa. Kwa hiyo . . . " Na, kisha, hiyo ni miaka yangu tu . . . Sihesabu ile ambayo hasa, nilizaliwa kimaumbile, na kimwili, ninahesabu tu miaka yangu ya kiroho, mnaona. Yapata miaka ishirini na minne iliyopita, nilizaliwa upya. Na, huo, huo ni wa Milele. Nayo itaninii . . . Ni siku moja kuu, ya kuzaliwa. Nayo kamwe haitaisha, hilo ni jambo moja hakika.

12 Sasa, ninataka Dada Gertie, kama ataweza . . . kabla hatujawaleta watoto kwa ajili ya kuwekwa wakfu watoto. Sasa, mara nyingi . . .

13 Katika Biblia, tunaona, mahali pekee nipajuapo, katika Maandiko, ambapo utaratibu, wa watoto. Sasa, watu wengi huwanyunyizia, mwajua, na kukuita ubatizo, na kadhalika. Ambalo, hilo ni—hilo ni sawa. Lakini mara nyingi mimi hujaribu tu, kama kusema jinsi Biblia isemavyo, mwajua. Na katika Biblia, kamwe hawakubatiza watoto wachanga. Wala hawakuwanyunyizia. Waliwaleta tu kwa Bwana wetu, Naye akawachukua mikononi Mwake, akawabariki, na kusema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie, kwa kuwa walio kama hao Ufalme wa Mbinguni ni wao."

14 Na jambo la kushangaza lilikuwa ni kwamba, sasa, nilifungua tu moja kwa moja kwenye Biblia, hasa mahali hilo lilipo, Marko 10. Hii hapa tu, moja kwa moja mbele zangu.

15 Basi kwa hiyo, Bwana, aliwaleta watoto wadogo... Waliwaleta watoto wadogo Kwake, Naye akawabariki tu, na kusema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwakataze, kwa kuwa walio kama hao Ufalme ni wao."

16 Sasa, tunajua ya kwamba Bwana wetu ameenda Utukufuni, na Roho Wake amerudi Kanisani, kuendeleza Ujumbe mpaka atakapokuja tena. Tunatazamia hilo.

17 Na jinsi tunavyolifanya hapa, ni kuwaleta tu watoto wadogo, na tunawaleta wazee wa kanisa, nami ninachukua watoto hao wadogo na kuwaweka wakfu kwa Bwana. Nafikiri ni ibada ndogo ya kupendeza sana, kuwaona hao jamaa wadogo. Maana, ni, haijalishi jinsi tulivyo wadogo, jinsi tulivyo wakubwa, mmoja wa hao jamaa wadogo ana mahali moyoni mwetu. Hiyo si ni kweli?

18 Sasa, tunapomjia Mungu, hivyo ndivyo tu tulivyo moyoni mwa Mungu. Kamwe hatutoki mahali hapo. Daima sisi ni watoto wadogo.

19 Ibrahimu alipokuwa na umri wa miaka tisini na tisa, alikuwa angali mtoto mdogo tu, kwa Mungu. Mungu alimwambia, akasema, "Mimi ndimi titi unalonyonya, Ibrahimu. Unaona, e—egemea tu Kwangu, ukanyonye, na kila kitu kitakuwa sawa." Ndipo akambadilisha Ibrahimu kuwa kijana tena, kwa kulishikilia tu Neno Lake.

20 Nami ninaamini tuliimba wimbo mdogo, wa *Waleteni*. Basi waleteni watoto wenu hapa juu sasa, enyi mnaotaka kuwaweka wakfu. Nitaomba wazee kama watakuja mbele, pia. Vema.

> . . . waleteni,
> Waleteni kutoka maeneo ya dhambi;
> Waleteni, waleteni,
> Waleteni wanaotangatanga kwa Yesu.

21 Loo, jinsi ninavyopenda kuwaona jamaa hawa wadogo! Sasa, jina lako na—nani? [Ndugu Riddle anasema, "Riddle."—Mh.] Jina lake nani? ["Sharon Louise."] Mtoto Sharon Louise Riddle. Nami nina hakika tunawapenda Ndugu na Dada Riddle. Tunamjua Ndugu Riddle hapa. Yeye ana duka la viatu hapa mjini. Nao wana mtoto mrembo sana hapa, mtoto Sharon, Sharon Louise, Sharon Louise Riddle. Ana umri gani, Ndugu na Dada Riddle? [Ndugu Riddle anasema, "Miezi minne."] Miezi minne. Jamani, jamani! Huyo ni maskini kipenzi cha moyo, sivyo?

22 Basi, sasa, Bwana amewapa huyu mtoto wa kupendeza, na sasa mnamweka wakfu Kwake, mkimweka mkononi Mwake, kwamba Mungu, Yeye aliyewapa, mnamrudisha Kwake. Mkimpa

Yeye, ili aweze kuyabariki maskini maisha yake na kuyafanya maisha ya utumishi. Na kumfanya. . . Ombeni ya kwamba Mungu atamfanya mtoto ambaye ataubariki moyo wenu mnapozeeka, na kama Yesu akikawia, na awe mtumishi mashuhuri wa Mungu. Nanyi mtamjivunia maskini msichana huyu. Mungu na alijalie sasa tunapomchukua, kumbariki.

23 Ninawataka wanawake wote, na, bila shaka, wanaume, pia, wamwangalie maskini mtoto huyu wa kupendeza. Hilo si ni zuri? Mtoto Sharon.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

24 Baba yetu mbarikiwa wa Mbinguni, katika Neno la thamani tunasoma ya kwamba walikuletea Wewe watoto wadogo, ili uweze kuweka mikono Yako juu yao na kuwabariki. Na sasa, huyu mume na mke, asubuhi ya leo, ndoa hii takatifu, Wewe umeweka chini ya ulinzi wao, mtoto huyu wa kupendeza, mtoto Sharon Riddle. Nasi tunaomba, mpendwa Baba wa Mbinguni, kwamba Wewe utambariki mtoto huyu, kwa kuwa wanakuja asubuhi ya leo kuweka wakfu, kumrudisha mtoto huyu Kwake Yeye aliyewapa. Nami ninakuomba Wewe, Mungu, kuwabariki, yabariki maisha yao. Pia jalia mtoto huyu mdogo, aishi, akue na awe na afya kamili, na awe mtumishi Wako. Pia umjalie awe mwanamke ambaye ataupendeza moyo wa Mungu, na mo—moyo wa mzazi. Lijalie, Bwana.

25 Basi sasa, kama mzee Wako, tunamwinua mtoto huyu Kwako, kama walivyomweka mikononi mwangu, nami namwinua Kwako. Katika Jina la Kristo, naomba umbariki mtoto huyu. Pia mjalie aishi na kukua, na awe mwenye nguvu na afya, na mtumishi wa Mungu. Tunaomba haya tunapomkabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, maskini kipenzi. Wewe ni mtoto mdogo wa kupendeza sana.

26 Mungu awabariki, nyote wawili. Na ninaomba muwe na furaha tele katika kumlea msichana huyu mdogo.

Tutakuja tukishangilia, tukileta mavuno.

Leta mavuno, leta mavuno,
Tutakuja tukishangilia, tukileta mavuno;
Leta mavuno, leta mavuno,
Tutakuja tukishangilia, tukileta mavuno.

Si itakuwa ajabu wakati huo?

Sasa na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi, kwa ajili ya maombi.

27 Ee Mungu, uliyeumba mbingu na nchi, hebu pumzi Lake lienende tu pamoja na Neno Lake, na kila kitu kimechukua mahali pake sahihi. Dunia, mwezi, nyota, zote ziliingia upesi mahali pao, mara tu Mungu alipolipulizia pumzi Neno Lake.

28 Basi, Ee Mungu, leo hii, tunaomba ya kwamba Wewe utalipulizia pumzi Neno Lako, kama tunavyojaribu kulileta kwa watu. Jalia lichukue mahali Pake, asubuhi ya leo, mahali Pake, na likite mizizi na kuimarika ndani ya kila moyo, ili kila mtu hapa aweze kupokea baraka Zako.

29 Wasaidie wale, Bwana, waliotoka njiani, waliodhoofika na kulemaa rohoni mwao. Nao hawakujui Wewe kama Mwokozi mpendwa, kama tulivyojaliwa kukujua. Tunaomba ya kwamba utawabariki kwa wingi, leo. Pia jalia wao, wanapoondoka kwenye jengo hili, wawe na furaha na kushangilia, juu ya Kristo aliyepatikana upya ambaye wamefahamiana naye kwenye mkutano huu.

30 Kama kuna wengine wanaoteleza, kwenye mahangaiko ya ulimwengu, Ee Mungu, warudishe. Na wagonjwa na wahitaji, Baba, tunawaombea, kwamba utamponya kila mgonjwa, leo. Watie moyo wale waliochoka. Na uwabariki wale wanaoshikilia kwa uaminifu. Tujalie, Bwana. Roho Wako na awe juu ya wote.

31 Libariki Neno linapotolewa; mnenaji atakayelinena, na msikilizaji atakayelisikia. Na, kwa jumla, upate utukufu kwa ajili ya kusanyiko hili asubuhi ya leo, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

32 Sasa, sijapumzika hasa kutokana na mkutano mrefu, ambao umekuwa sasa yapata miezi minne, na majuma haya matano yaliyopita yamekuwa ya kuchosha sana. Kwani, tumekuwa na mkutano mzuri sana kote nchini, sasa, kuanzia New York hadi San Francisco; taifa lote, tukienda huku na huku, mbele nyuma, jinsi tulivyoenenda. Naye Bwana ameokoa mamia mengi, mengi ya watu.

33 Jumapili iliyopita, juma moja lililopita, pekee, Baba yetu wa Mbinguni mwenye baraka, niliona kati ya elfu moja, hadi elfu moja mia tano, wenye dhambi wakitubu kwa wakati mmoja, madhabahuni, huko Oakland, California, katika uwanja mkubwa. Ilikuwa imejaa kabisa. Na ilitubidi—ilitubidi kuketi katikati ya mahali chini katikati, badala ya ka—kandokando za uwanja. Na Bwana akabariki tu.

34 Na tulikuwa, mle ndani, na tetemeko kubwa la nchi, kama mlivyosikia. Na huo ulikuwa wa kwanza kwa mke wangu kuwa ndani. Alikuwa kidogo ameshtuka, baadaye. Lilikuwa na nguvu sana, hata jengo likatetemeka, na vumbi likapeperushwa, na chupa kwenye. . . Tulikuwa tumesimama kwenye duka la dawa, tukichukua postikadi ili kutuma nyumbani, nazo chupa zikatikisika, na chemli ikaanguka. Na majengo makubwa yakatikisika; barabara zikapasuka, na sehemu yake ikazama chini. Basi inatukumbusha tu kwamba maandiko ya mkono yako ukutani. "Kutakuwa na matetemeko ya nchi mahali mahali."

35 Katika siku hiyo moja, matetemeko manane ya nchi yaliupiga mji uo huo. Na ndipo yapata saa nne usiku huo,

tulikuwa tu tumeingia, ama saa nne na nusu, na kuenda kulala; nayo ta—taa, ikiwa katikati ya sakafu, karibu ianguke, kutokana na tetemeko jingine la nchi, lenye nguvu. Inaonyesha tu, ya kwamba maili mia nane chini yetu, hakuna chochote ila moto, lava nyekundu.

36 Na ilikuwa tu kwenye wakati, na tuliwasikia wachokozi (wetu) ng'ambo ya bahari, wakisema ya kwamba wanawazuia watu wasiende Scandinavia, na kadhalika, kwamba wangewaangamiza kwa silaha za atomiki. Basi tunashangaa ni nini kingefanyika iwapo wangeanza kuangusha mabomu hayo na kulipua sehemu hizo ardhini. Wakati, ingefanya tu hasa kile Mungu alisema ingefanya. "Hakuna maji tena, bali moto wakati huu."

37 Hivyo basi, inaleta furaha moyoni mwa yule anayekungojea Kuja kwa Bwana, na saa yenye baraka wakati miili hii dhaifu itakapobadilishwa na kufanywa kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu. Nasi tutamwona. Hakuna kusumbuka tena, hakuna huzuni tena, hakuna uzee, hakuna siku zisizo na kikomo, hakuna njaa tena, hakuna fadhaa tena, hakuna ugonjwa tena, hakuna mauti tena.

38 Loo, hatuwezi kabisa kuelewa! Nakwambia, ewe rafiki! Ni ngumu kwa sababu sisi ni binadamu, na mauti ni kitu ambacho sote tunachukia kukabiliana nacho. Lakini ni—ni faraja iliyobarikiwa, ni kitu kilichobarikiwa, kujua kwamba Yeye atakuja siku moja, nayo mambo haya yatabadilishwa.

39 Sasa, kumbukeni, na mwingie katika ninii yenu. . .hasa nyinyi marafiki wenye dhambi, sasa, mweze kuja mkutanoni, uamsho huu unaokuja.

40 Sasa, kwa njia tu ya kuzungumza, koo langu, kama nilivyosema, halijawa sawa, bado, hasa, na ningali mchovu kidogo. Lakini, nimepumzika, juma hili, nimejiepusha hata na simu na kila kitu, ili niweze kuwa na siku chache kupumzika.

41 Na kisha, juma hili lijalo, ninataka kupumzika kidogo, nikiweza, na kisha nijitayarishe kwa ajili ya maskini uamsho huo. Halafu niende Canada, na kutoka Canada nirudi Indianapolis. Kutoka Indianapolis ndipo niende Chicago. Na kutoka Chicago. . .Huo ni Mkutano mkubwa wa Kimataifa wa Wafanyabiashara Wakristo. Nao wamenishika. Sasa, nyinyi niombeeni, na hasa kwenye wakati huu wa uamsho, ili Mungu aniongoze. Ziara kamili ya ulimwenguni kote itaanza Juni, na kurudi Novemba, ama Julai, hasa. Na hiyo ni kwenda Ulaya, Asia, kote kupitia visiwani, bahari, na kurudi kote, kupitia Pwani ya Magharibi. Tuondoke mashariki, na kuzunguka kote duniani, turudi Magharibi. Wakati wa uhitaji ulioje!

42 Basi sasa kuna kitu kinachonizuia kidogo kwa namna fulani. Sijui kama ni kitu kilichoko njiani, ama nini, sijui. Lakini,

nyinyi niombeeni, naye Mungu kwa hakika atakishughulikia sawasawa.

43 Sasa, ninazo sehemu mbili katika Maandiko ambazo nimechagua asubuhi ya leo kusoma, kwa sababu hii, kwamba watu wanakuja, wanapaswa kuombewa. Huu ni muda mfupi tu wa kuwaombea wagonjwa na wahitaji. Nami ningependa tu kufundisha kidogo juu ya Neno.

44 Halafu, labda, Bwana akipenda, usiku wa leo, huenda nisifundishe tu, bali nihubiri kidogo kutoka kwenye Neno.

45 Sasa ninataka kusoma kutoka sehemu mbili, na hiyo ni katika Agano la Kale, sehemu zote mbili. Moja katika Hesabu, mlango wa 13, na ki—kifungu cha 30. Na nyingine ni katika Yoshua, mlango wa kwanza, na kifungu cha 9.

> *Kalebu akawatuliza watu mbele ya Musa, akasema, Na tupande mara, tukaitamalaki; maana twaweza kushinda bila shaka.*

46 Na halafu katika Yoshua, kifungu cha 9 cha mlango wa kwanza.

> *Je, si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike: kwa kuwa BWANA, Mungu wako, yu pamoja nawe* kila *uendako.*

47 Basi Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake. Nalipenda tu Neno. Na kama ningesema kwa ajili ya somo, asubuhi ya leo, ninataka kuchukua ili kupata muktadha humu, kifungu, kiitwacho: *Mungu Hutimiza Neno Lake*. Sasa, ni. . . Tunaweza tu kukaa juu ya hilo kwa wiki kadhaa; tufanye uamsho wa mwaka mmoja na bado uwe safi tu mwishoni kama ulivyokuwa mwanzoni, ya somo hilo, la, *Mungu Hutimiza Neno Lake*.

48 Kuna jambo moja ambalo Mungu hawezi kufanya. Je, uliwahi kuwazia hilo? Kuna jambo moja ambalo Mungu hawezi kufanya, hilo ni kushindwa. Anaweza kufanya kila kitu ila kushindwa, lakini hawezi kushindwa. Kwa hiyo, kama tumaini letu takatifu sana limejengwa, asubuhi ya leo, juu ya Yule wa ajabu Ambaye anaweza kufanya lolote lililopo kufanywa, isipokuwa kushindwa, tunapaswa kuwa na ujasiri kiasi gani katika Neno Lake la Milele!

49 Moyo wangu umechochewa katika mwaka uliopita, baada ya kutazama katika mataifa na kuona mambo yanalundikana, jinsi yanavyolundikana, na itikadi ndogondogo zikiinuka. Inanikumbusha vizuri kile kilichoandikwa hapo kwenye jiwe hilo la msingi, asubuhi ile tulipoweka wakfu. . . au tulipoweka jiwe la msingi. Bwana aliponiamsha; bila kujua maono yalikuwa nini, katika siku hizo.

50 Ninatazama dohani juu ya nyumba, futi tano ama zaidi kutoka pale nilipokuwa nimeketi wakati ono lilipotokea, miaka

ishirini na mitatu iliyopita, mwaka wa 1933. Ni kama miaka ishirini na minne iliyopita, nadhani. Ninaitazama dohani sasa hivi.

51 Ilikuwa muda mrefu kabla sijaoa. Nilikuwa sina mwenzi, na nyumbani. Tulikuwa tu tunajenga kanisa hili. Nasi tulikuwa tunaweka jiwe la msingi asubuhi hiyo, wakati Bwana aliponipa ono hilo. Nilikuwa nimeamka na kuchungulia dirishani. Na ilikuwa ni mwezi Juni, na maua yenye manukato, au matumba yakichipuka. Na ilionekana kana kwamba nilitoka nje, ama kitu fulani. Ndipo ni—nikamwona Bwana Yesu, na nikaona maskani yangu. Naye akaniambia ya kuwa hii si maskani yangu; na kuniweka chini ya anga. Wengi wenu mnajua ono hilo, kwa sababu limeandikwa na kuchapishwa, na ninaamini toleo la nne au la tano, la vitabu karibu laki moja vimeenda katika lugha kumi na saba tofauti. Na angalia tu jinsi hilo limetimia, neno kwa neno, halikushindwa kamwe! Jinsi tulivyokusanyika pamoja katika kundi dogo la kupendeza la watu, na jinsi Bwana alivyotubariki, halafu kutoka mahali hadi mahali, lakini hatimaye kwenye nyanja za uinjilisti, na ulimwenguni kote sasa, jinsi mambo yalivyoenda.

52 Na jinsi wakati umefika kwamba—kwamba ingekuwa mambo haya yametukia. Jinsi ambavyo ulimwengu ungekusanya waalimu, wenye masikio ya utafiti, na Kweli ingekataliwa na ingegeuzwa kuwa hadithi. Na kisha jinsi ambavyo Yeye alisema, "Lihubiri Neno. Dumu kwenye Neno." Na kama jambo lolote ambalo nimejaribu kufanya, ni kudumu kwenye Neno la Milele la Mungu.

53 Tunaishi katika saa za mwisho za kipindi hiki cha ulimwengu. Sioni jinsi mtu yeyote angeweza kuangalia, kuangalia tu magazeti, au kufungua redio, na asitubu. Si—siwezi kuiona. Jinsi tulivyo tu kwenye m—mkesha wa jambo fulani kuu ambalo linakaribia kutokea. Hata maumbile yanaonyesha hilo. Dunia inazidi kuwa na woga. Inalipusha volkeno zake, nayo ina—ina unyong'onyevu wa hofu. Matetemeko makubwa ya ardhi yanatikisika na kuzipasua njia, na mambo ya kutisha ya sahani zinazoruka, na makombora ambayo wanaweza kurusha duniani, na kuharibu, kuangamiza taifa katika dakika tano. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Kitu kinachukua . . . Hakuna njia ya kukizuia. Hakuna njia. Kuna njia moja tu ya kutoka kwake, na hiyo ni juu. Hakuna njia ya kujaribu kujificha. Hakuna mahali pa kujificha ila pamoja.

54 Kama vile wasichana wadogo walivyokuwa wakiimba hapa, nilipokuwa tu mhubiri mvulana, walikuwa wakiimba:

> Hakuna mahali pa kujificha hapa chini.
> Nilikwenda kwenye miamba ili kuficha uso wangu,
> Lakini miamba ilipiga kelele,

"Hakuna mahali pa kujificha hapa chini."

55 Lakini kuna Mahali pa kujificha. "Jina la Bwana ni ngome imara: wenye haki huikimbilia, wakawa salama." Jinsi tulivyo na furaha kuwa na Mahali hapa pa kujificha, katika wakati wa mwisho.

56 Na tunapotazama huku na huko na kuona ishara hizi kuu zikifanya kazi, na uamsho huu unaokuja, Mungu akipenda, ninataka kwenda mpaka kwenye Mwanzo, na kuleta mambo hayo makuu ya kuvutia, ambayo, "Tuko mwisho. Tuko hapa." Ninaamini ya kwamba kizazi hiki kilichopo, kiko duniani sasa hivi, ambacho kitaona Kuja kwa Bwana Yesu. Nina umri wa miaka arobaini na nane. Huenda nisiione. Sijui. Inaweza kuja kesho. Lakini, ninaamini ya kwamba kuna wengine hapa ambao wataona Kuja kwa Yule Mwenye Haki, mwisho wa wakati. Nami naamini ya kwamba wengi wetu, hasa tulio katika kanisa hili asubuhi ya leo, kamwe hatutakufa kwa uzee, mpaka tuone moja ya mambo ya kutisha sana yakitukia, ambayo yamewahi kuwapata watu, yatakayotokea hapa katika taifa hili. Ni ukweli.

57 Ndugu, tumevuka mipaka ya rehema mpaka hakuna kilichosalia ila hukumu, lakini mwenye haki haitambidi kuadhibiwa pamoja na wasio haki. Mungu atakuja, na Yesu atalikomboa Kanisa Lake, nasi tutapanda juu hewani kumlaki. Na itakuwa mbali zaidi ya mabomu yoyote au shida zozote, nasi tutalindwa wakati huo.

58 Kwa hiyo, wanangu, mrudieni Mungu wenu, upesi. Usibishane na ulimwengu kwa chochote. Jiepushe na ulimwengu huu wa kisasa. Jiepushe na hizi theolojia za kisasa. Mwangalie tu Mwanakondoo wa Mungu. Soma Biblia yako na uombe, wakati wote. Usichoke. Shangilieni, mfurahie, kwa maana ukombozi wa Kanisa unakaribia, tutakapomwona Yeye Yule aliyekufa kwa ajili yetu.

59 Somo letu ni mpangilio unaofanana kwa namna fulani na enzi ya leo. Kwanza kabisa, Maandiko ya kwanza, nilikuwa nikisoma katika Hesabu. Yalikuwa yanazungumza juu ya watu ambao walikuwa wameitwa kutoka katika taifa kubwa, lenye nguvu waliokuwa karibu, na walikuwa wamepokea hukumu yao.

60 Nataka mwelewe kwamba dhambi haitakosa kuadhibiwa, bila kujali, ni katika taifa, au kanisa, au nyumba, au mtu binafsi. Dhambi lazima ishughulikiwe kwa msingi wa hukumu. Hakuna njia nyingine. Haiwezi kupatanishwa, useme, "Nilifanya vibaya, sasa nitafanya vizuri." Hiyo haitafanya kazi. Huwezi kufanya upatanisho, wewe mwenyewe, kwa sababu upatanisho tayari umefanywa.

61 Ni maungamo, ya kwamba umekosea, halafu uje na unyooshe.

62 Kwa hiyo, dhambi lazima ishughulikiwe, na Mungu daima hushughulika na dhambi kwa hukumu. Hiyo ndiyo sababu Bwana wetu alikufa kifo alichokufa, pale Kalvari, ni kwa sababu hiyo dhambi ilikuwa ni kitu kibaya sana, kwamba hukumu ya dhambi iliwekwa juu Yake. Ili wale wanaotamani, wawe huru, kwa kumwamini Yeye na kumkubali Yeye kama kizuizi chao cha dhambi zao. Si jinsi tunavyoweza kuwa wema, bali jinsi tunavyomwamini Yeye na kumkubali. Na tunapomkubali, Yeye huja ndani ya mioyo yetu, na hapo ndipo sehemu nzuri ilipo. Si juu ya kile ambacho tunaweza kufanya; ni juu ya kile alichokifanya Yeye, na kile ambacho ametufanyia. Hapo ndipo, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kuchubuliwa kwa maovu yetu, na adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

63 Sasa, watu hawa walikuwa wamekaa huko Misri yapata miaka mia nne. Na sisi sote tunafahamu kule kushuka kukuu kwa wana wa Israeli, na jinsi ambavyo, kule chini, Mungu alikuwa amewakabidhi kwa Wamisri. Nao walikuwa wamewatendea vibaya, kwa maana Neno la Mungu lilisema wangefanya hivyo.

64 Sasa, Mungu alimwahidi Ibrahimu, miaka mia nne, ya kwamba watu wake wangekaa ugenini katika nchi ya kigeni. Na wakati wa ahadi ulipokaribia, Mungu ana kila kitu tayari kutimiza.

65 Loo, ninapenda tu jambo hilo, ninapowazia jambo hilo. Kwa wakati muhimu tu! Hachelewi hata dakika moja. Yeye daima yuko kwa wakati. Laiti tungaliweza kuwa hivyo! Loo, tunajaribu kusukuma jambo hilo. Tunajaribu kulifanya wakati wetu. Lakini hatuwezi kamwe kufanya hivyo. Mungu hufanya kwa wakati Wake. Hatuwezi kulifanya liwe tofauti.

66 Jana, nikiwa nimesimama katika uga wa—wa dada yangu anayeishi karibu nasi, Dada Wood, tulikuwa tunaona kifukofuko kidogo ambacho kilikuwa kimejiundia juu ya mti. Na upepo ulikuwa ukikipeperusha huko na huko. Naye alikuwa akiiambia, ya kwamba, katika Vijito Vya Majangwa, ninaamini, kwamba alikuwa akisoma makala kuhusu kifukofuko. Ni mdudu mdogo anayeingia huko na kuunda ganda dogo kumzunguka, ili kumlinda wakati wa baridi. Na, lakini ukifika wakati . . .

67 Mtu huyu ambaye alikuwa akishughulika na yule jamaa mdogo, walimwona maskini kifukofuko huyo akitembea na kuyumbayumba. Nao walimhurumia sana jamaa huyo mdogo, kwa hiyo wakafikiri wangekata tu mwisho wake na kuacha maskini mdudu huyo atoke. Kwa sababu, alipotoka pale, alikuwa anaenda kuwa na mbawa. Aliingia kama mdudu, au mdudu mdogo, anatoka nje na mbawa, katika hali kama ya utukufu zaidi. Naye alipokuwa akitetemeka, na kuvuta, na kuvuta, na kupiga, na kuuma, na kujaribu kutoka nje ya kifukofuko,

walimwonea huruma. Kwa hivyo walidhani wangempa njia ya mkato tu, kwa hivyo wanaenda na kuchukua mkasi na kukata mwisho. Na walipokata mwisho, maskini mdudu huyo akatoka. Lakini kamwe hakuwa sawa, kwa sababu hakuwa na nguvu yoyote katika mwili wake. Hakuwa na . . . Hakuweza kutumia mabawa yake.

68 Nami nafikiri hivyo ndivyo tumejaribu kulirudia, tunasema, "Shuka kwenye madhabahu!" Na—na kusema *hili, lile,* ama *lingine,* na kujaribu kuwarudisha watu kwa Mungu, ama kanisani, ama kumjia Kristo. Waache tu wapige yowe na kuitoa. Ni hayo tu. Fanya tu njia yako kutoka kwayo. Ni hayo tu. Ukijaribu kuwapa njia ya mkato, hawawezi kusimama kamwe. Ninapenda tu kuwaona wakijitahidi na kuifanyia kazi mpaka Mungu awape Kuzaliwa halisi, kwa njia ya kawaida, wape tu Kuzaliwa halisi. Ninii tu . . .

Watu wanasema, "Vema, mpenzi, nadhani umeomba vya kutosha."

69 Wewe kaa tu hapo mpaka uwe tayari kuruka. Hilo ndilo jambo pekee. Mungu ana njia ya kufanya hivyo.

70 "Loo, vema, ukitaka kuwa mzuri, nenda tu ujiunge na kanisa. Mama aliienda kanisa lilo hilo."

71 Hiyo inaweza kuwa sawa tu. Lakini, unajua, inahitaji kifo kuleta uhai. Nasi hatuna budi kufa, mpaka, basi, tumekufa sana hata kunaweza kuwa na Uhai mpya unaoingia. Kisha mbawa zetu zitakuwa za thamani; na u—uzoefu wetu, tulio nao, utakuwa wa thamani kwa wengine na kwetu sisi wenyewe.

72 Israeli haikuwa tayari. Lakini Mungu alikuwa tayari. Naye alikuwa na mtoto mchanga aliyezaliwa, jina lake Musa. Naye alikuwa pale pale, akiwa na umri wa miaka arobaini, kuwatoa hao watoto, lakini Israeli hawakuwa tayari. Na kwa sababu hawakuwa tayari, basi iliwabidi kufanya kazi miaka ishirini zaidi, ama miaka arobaini zaidi, ilikuwa. Miaka arobaini zaidi, iliwabidi ku—kufanya kazi kwa taabu, huko chini Misri. Wakati, wangeweza kutoka, miaka arobaini kabla ya hapo, kama tu wangekuwa tayari.

73 Mungu alikuwa tayari, kwa sababu wakati wa ahadi ulikuwa umekaribia. Mungu alimtuma Malaika duniani, kuwatayarisha watu, kutimiza Neno Lake, kwa maana Mungu daima hulitimiza Neno Lake. Alimwambia Musa, "Nimeyaona mateso ya watu Wangu, nami nimesikia kuugua kwao na vilio vyao kwa sababu ya wasimamizi wa kazi. Na nimekumbuka. Nimelikumbuka Neno Langu, ahadi Yangu." Miaka mia nne ilikuwa imepita, lakini Mungu angali alikumbuka Neno Lake.

74 Karibu miaka elfu mbili imepita, lakini Mungu angali analikumbuka Neno Lake. "Nitakuja tena na kuwakaribisha Kwangu; ili nilipo mimi, nanyi pia mwepo." Nami ninaamini wakati wa ahadi unakaribia.

75 Angalieni. Alipokuwa akizungumza na kujiandaa, na miaka mia nne ilikuwa imepita, na Mungu alikuwa kwenye wakati ufaao na Neno Lake. Basi tunagundua kwamba. . . baada ya miaka arobaini zaidi.

76 Na huenda nisimame hapa kusema maneno haya. Sasa unaweza kuninukuu, kwa maana ninajua inarekodiwa huko nyuma. Ninaamini kwamba sisi ni. . . Kuja kwa Bwana Yesu kumepita wakati wake kwa mbali. Ninaamini kulistahili kuwa muda mrefu uliopita. Lakini, ni kwa sababu ya Kanisa, haliko tayari kukutana Naye.

77 Sasa, kama utatambua, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Katika siku za Nuhu, kabla ya gharika, jinsi ingekuwa. Na Mungu hakutaka yeyote apotee, bali kwamba wote wafikie toba, ndipo aliteseka kwa muda mrefu. Hatua ya mafuriko ilikuwa imepita wakati wake. Huko Misri, ilikuwa imepita. Je, mnaipata? Katika uharibifu wa kabla ya gharika sasa; imepita kwa mbali, uharibifu katika hukumu. Na kutoka Misri; muda uliopita, miaka arobaini ya nyongeza.

78 Lakini Mungu alikusudia. Mungu alikusudia kwamba Neno Lake lisingemrudia. Alikuwa anaenda kulitimiza Neno Lake. Yeye hana budi kulitimiza Neno Lake. Yeye hana budi kufanya jambo hilo, kusudi awe Mungu. Ikibidi afanye ba—badiliko la kila kitu, na, kwa neema atafanya hivyo.

79 Hiyo ndiyo sababu ninasema. . . kama Kanisa halitajifanya Mwenyewe tayari. Hilo ni jukumu lako, kujiandaa. "Bibi-arusi amejiweka tayari Mwenyewe." Mavazi yamelipiwa. Yako tayari, lakini lazima uwe tayari kuvaa mavazi hayo. "Kanisa limejiweka Lenyewe tayari."

80 Sasa, ndugu, sikilizeni. Kama Kanisa halitajitayarisha, Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Ikiwa watu hawa wa utakatifu hawatajiweka sawa, na kurudi kazini tena, kurudi kwenye Injili, Mungu atainua kutoka kwenye. . . Anaweza kuleta Wakatoliki, Wapresbiteri, au chochote anachotaka. Atafanya hivyo.

81 Majuma machache yaliyopita, huko Lima, Ohio. Wengi, baadhi yenu, mmeketi hapa sasa, waliokuwepo. Miongoni mwa Wapresbiteri, Wabaptisti, na Wamethodisti, walimiminika madhabahuni. Walipokea na kuitikia Injili, bora zaidi, bora zaidi kuliko, mara nyingi, yale watu wa utakatifu wafanyayo. Tumeiweka tu akilini mwetu, ya kwamba tumeitwa kwa Jina Lake takatifu, na kuiacha iende hivyo. Inamaanisha zaidi ya kuitwa kwa Jina Lake. Inamaanisha kuishi kwa ajili Yake Yeye aliyekufa kwa ajili yako. Ni maisha, maisha yaliyowekwa wakfu kwa Mungu. Loo, jinsi tunavyohitaji, kurudi kwenye Biblia!

82 Hapa siku chache zilizopita usiku, nilikuwa nikiwaambia Walutheri, ambapo. . . kwenye mkutano huko juu. Sasa ndiyo kwanza waseme, "Tupe vyuo vingine vitano kama hivi, vya hao

Walutheri, kwamba sabini na mmoja wao walimpokea Roho Mtakatifu siku ile chuoni," nilipokuwa huko. Wakasema, "Tupe shule zingine tano kama hizo, na Bwana akawie miaka kumi, kanisa lote la Kilutheri litajazwa na Roho Mtakatifu." Loo, jamani! Hakika.

83 Mungu anaweza, kwa mawe haya! Ataleta Kanisa liwasilishwe, lisilo na doa, wala kunyanzi, wala dosari. Neema Yake inatosha kabisa, na anaweza kufanya mengi, zaidi.

84 Nami nikasema, hapa si muda mrefu uliopita, Walutheri walikuwa na nuru ya kurunzi kwa ulimwengu. Nini ilitokea? Kama mlikuwa nuru ya ulimwengu, ninyi Walutheri, wakati mmoja, katika matengenezo ya kwanza, nini kilifanyikia nuru yenu? Je, ilizimika? Hii ndiyo sababu ilizimika, ni kwa sababu mliacha Neno la Mungu. Mliamini kwamba, "Mwenye haki anapaswa kuishi kwa imani," ambayo ni Kweli kabisa. Lakini kuna zaidi ya hayo, "Mwenye haki ataishi kwa imani."

85 Kisha wakaja Methodisti. Wao, ninyi Wamethodisti, mlichukua mwanga wa tochi ya utakaso, nanyi mlishikilia hiyo nuru ya tochi kwa ajili ya uamsho mkuu. Hiyo yote ni kweli. Lakini, nini kilitokea, ni nini kilitendeka kwa kanisa la Methodisti? Ni kwa sababu mmeiacha nuru izimike. Hicho ndicho kilichotokea. Nanyi mlihubiri utakaso, kazi ya pili ya hakika ya neema, ambayo ni ya hakika, Kweli, kwa Biblia, bali nyinyi mliiacha tu iende hivyo.

86 Na kisha wakaja Wapentekoste, pamoja na kurejeshwa kwa karama. Nanyi mkanena kwa lugha, na kisha mkaunda fundisho kutokana na hilo. Na kisha nini kilitokea? Nuru yenu imezimika. Kuna nini? Ni kwa sababu mnakosa kudumu na Neno.

87 Neno la Mungu tunalifunua, na lazima tufunue Neno la Mungu linavyofunuliwa.

88 Kadiri wakati unavyosonga, sayansi inakuwa wazi. Na ikiwa ulimwengu wa asili. . .Mtu huyu ni mtu yule yule aliyekuwa miaka elfu sita iliyopita, wakati Mungu alipomwumba. Yeye ni mwenye akili yule yule. Yeye ni akili ile ile. Yeye ni mtu yule yule tu, mwenye hisi zile zile tano, aliyekuwa maelfu ya miaka iliyopita. Lakini tazama ni maendeleo gani amefanya katika miaka hamsini iliyopita. Angalia kile huyo mwana wa Mungu aliyeanguka amefanya. Amevumbua magari, na redio, na taa za umeme, na mabomu ya atomiki, na ndege za jeti. Angalia jinsi ilivyo haraka. Kurasa zinageuka haraka katika sayansi.

89 Lakini tunajaribu kukaa nyuma kwenye kanuni fulani ya imani ya zamani ya kanisa, na kusimama pale, wakati Mungu anapotutaka tulifunue Neno. Tunaishi katika siku ya mwisho. Tunaishi katika wakati ambapo Kanisa kuu la kupendeza la Mungu linapaswa kuwa limesimama kwa miguu Yake, liking'aa kama Yungiyungi la Bondeni.

90 Lakini tumerudi, wengine, “Vema, mimi ni mfuasi wa Presbiteri, Methodisti, Pentekoste. Mimi ni *hiki*, au *kile*.” Loo, aibu iliyoje!

91 Tunapaswa kufunua; Roho ya Mungu ikimiminika. Si kibubujiko kimoja tu kidogo, si ubatizo mmoja mdogo; lakini, ubatizo baada ya ubatizo! Sio ufunuo, “mwenye haki ataishi kwa imani,” au, “utakaso,” au, “karama za Roho.” Lakini, ufunuo baada ya ufunuo, nguvu baada ya nguvu, utukufu baada ya utukufu! Mbona, tunapaswa kuwa juu sana, tayari kwa uhamisho. Nasi tunakawia nyuma katika mambo ya kale, na kusema, “Vema?” Tunaendelea kurudi nyuma. Twende mbele!

92 Waebrania hao walisema, “Sasa, hapa, tunalishwa vizuri sana, ingawa tunafanya kazi kwa bidii. Na sasa tuna vitu tulivyo navyo, tuna vyungu vya kitunguu saumu, na kadhalika, kwa hiyo na turidhike.”

93 Lakini, Musa alikuwa na ufunuo. Alikuwa amekuwa katika Uwepo wa Mungu. Alikuwa na kitu kingine. Alirudi na kuwaonyesha ya kwamba Mungu yule yule aliyekuwepo mamia mengi ya miaka kabla ya hapo, alikuwa ni Mungu yeye yule. Naye alifanya ishara na maajabu mbele yao, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu yeye yule.

94 Loo, Jina Lake na libarikiwe! “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Vizazi vinabadilika, nyakati zinabadilika, watu wanabadilika. Lakini, Mungu anabaki. Hana budi kuwa yule yule, wakati wote. Neno Lake ni Kweli ya Milele. Hawezi kuliondokea Hilo, kutoka kulia au kushoto. Lazima abaki vile vile.

95 Kisha tunapata kile kinachotokea. Huyu hapa Musa anashuka, akiwa na ishara. “Nimekuwa katika Uwepo wa Mungu. Nimemwona Mungu, na Mungu amefanya mambo makuu.” Alifanya tendo la uponyaji wa Kiungu. Alifanya kitendo kingine, kama mwujiza. Naye akawaonyesha ya kwamba Mungu yule yule wa Mbinguni alikuwa amemtokea. Baada ya mamia ya miaka ya nguvu zisizo za kawaida kutoweka, alionyesha kwamba Mungu bado alikuwa hai.

96 Na Mungu alimtuma, na kusema, “Nenda ukawaambie kwamba ‘MIMI NIKO’ amekutuma.” Si “Nilikuwa” au “Nitakuwa.” “MIMI NIKO,” wakati uliopo! Yeye si “Nilikuwa.”

97 Jinsi watu wanavyoweza kudai Mungu, na kusema, “Siku za miujiza zimepita, na uponyaji wa Kiungu na baraka zote zimetoweka,” na bado waseme, “Yeye ndiye Mungu aliye hai, na MIMI NIKO”? Kama Yeye ni “MIMI NIKO,” Yeye ni halisi tu kama alivyokuwa kwenye kichaka kilichowaka moto.

98 Hilo Jina kuu alilotokea pale, hakuna mwanachuoni ambaye bado amepata kulifasiri, J-v-h-u. Hakuna mtu . . . Wanaliita “Yehova,” lakini halikuwa hivyo. Hakuna anayeweza kulifasiri.

99 Kwa nini? Ni Yule wa Milele. Amina. Anakaa katika Nuru. Anakaa katika Umilele. Anakaa katika hali ya kutokufa; milele "MIMI NIKO." Haleluya!

100 Imani yangu imetulia juu ya Mwamba huo imara. Hakuna kitu kinachoweza kudhuru wakati umetia nanga kwenye Mahali hapo. Dhoruba zinaweza kutikisa na kuipiga, lakini nanga yangu inashikilia ndani ya pazia. Wakati mwanamume au mwanamke ametia nanga na kuikubali. Hakuna kitu kinachoweza kukuyumbisha kutoka kwayo.

101 Kama vile wakati wao ulivyokuwa wa ukombozi, nao wakakosa kuuona, ndivyo ulivyo wakati wa ukombozi, amri za kuondoka kwa Kanisa. Umekaribia.

102 Angalia, rafiki yangu. Walikuwa na nini? Kwanza, Neno. Pili, nabii. Tatu, Malaika wa kuwaongoza, awaongoze. Kila mmoja alikubaliana na mwenzake; hao watatu. Neno lilikubaliana na nabii; naye nabii akakubaliana na Neno; Malaika alikubaliana na wote watatu, wote. Neno; nabii; Malaika! Walikuwa tayari kwa safari.

103 Loo, Jina la Bwana Mungu libarikiwe! Tuko kwenye wakati wa mwisho; Neno, nabii, na Malaika, wote watatu pamoja, ushuhuda mmoja mkuu. Mungu alisema kila wakati, "Kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu, kila neno na lithibitike." Naye nabii wa kweli daima atakubaliana na Neno; na Malaika yeyote atashuhudia Kweli. Amina. Tuko tayari kwa maagizo ya kuondoka. Hakika.

104 Naye akawatoa watu. Walipokuwa wakipanda, walianza kumwasi nabii, na kumwasi Malaika, na kumwasi Mungu, na kuliasi Neno. Na wakaingia kwenye matatizo. Biblia ilisema, "Kulikuwa na umati wa watu waliochanganyika waliokwenda pamoja nao." Umati wa watu waliochanganyika ulitoka.

105 Ilikuwa ni nini? Miujiza ilikuwa imefanywa. Kulikuwa na miujiza na maajabu. Mtu yeyote, mwanadamu, anatamani kuona nyuma ya pazia kutoka anakotoka, na kutoka kule atakakoenda siku moja. Anatamani kuona nyuma ya pazia. Lakini, mara nyingi, wakati matendo ya kimbinguni yamefanyika, basi kuna kundi mchanganyiko linaloenda.

106 Hilo ndilo lililotukia katika siku za Luther. Wakati mchanganyiko...Mungu amejaribu kuwatoa tangu siku hiyo. Na katika siku za Luther, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Waliijaribu, na kuijaribu, na kuona ni hivyo. Umati mchanganyiko ulikwenda. Na mara Luther alipoenda, kulifanyika nini? Waliingiza kanisa katika utaratibu na kutengeneza mfumo mkubwa sana wa kikanisa. Na walipofanya hivyo, kanisa lilirudi kwenye rafu.

107 Moja kwa moja akaja John Wesley, mmoja wa mashujaa wakuu, hodari wa wakati wa kati. Naye akatoka moja kwa moja na kuliasi kanisa la Kianglikana, na kuliasi kanisa Katoliki,

na kuuasi ulimwengu, kwamba, "Mungu mtakatifu alisema, 'Ni lazima watu waishi watakatifu!'" Naye alidumu kwenye ahadi Yake, ya ahadi ya Mungu, naye akaleta muujiza. Kukafanyika nini? Umati mchanganyiko ulienda naye. Na Wesley alipoenda, ndipo umati mchanganyiko ukaingia. Nao wamefanya nini? Wamelichafua kanisa, mpaka wengi wao hawatakuwa na nyimbo za "Damu" katika vitabu vyao vya tenzi. Hakika.

108 Vema, baada ya hayo wakaja Wapentekoste, nao Wapentekoste wakaanza kupata karama. Mara tu walipozifikia karama, jambo la kwanza . . . Karama ndogo zaidi katika kundi zima ni "kunena kwa lugha." Hiyo ndiyo ya mwisho na ndogo zaidi. Mungu aliwaanzisha na mambo madogo, na hawakuweza hata kushikilia hilo.

109 Tazama hapa. Karama ya kwanza, katika msururu wa karama, ni hekima; pili ni maarifa. Na ikiwa huna hekima yoyote, unajuaje la kufanya na maarifa? Tafuta mambo bora kwanza, hekima. Na kama huna hekima, unaweza kufanya nini na maarifa, ama kunena kwa lugha, ama mambo haya mengine? Inahitaji hekima. Inahitaji *hekima* ya Mungu. Sulemani alisema, "Iite mama yako." Kweli.

110 Lakini walifanya nini? Wapentekoste walipokea kunena kwa lugha, nao wakaunda madhehebu kutokana nayo. Nao wakaenda, wakasema, "Hii Ndiyo." Hakika, walifanya hivyo. Na umati mchanganyiko ukaenda pamoja nao.

111 Na, leo, nini kimewapata Wapentekoste? Kuna vikundi viwili kati yao. Kimoja ni baridi tu, na wa kawaida, na wagumu, na wenye ushupavu, wawezavyo kuwa. Na hicho kingine kinafuata lundo kubwa la itikadi; mafuta na damu kutoka mikononi mwao, na chochote kile, kote nchini, na kuziita shuhuda za Roho Mtakatifu; na vyura, na mijusi, na kadhalika, wakiruka kutoka kwa watu, na kisha kuyaweka kwenye kileo, na kadhalika. Mtu yeyote anajua kwamba shetani hana mwili wa nyama.

112 Na kama Damu ya Yesu Kristo ilimwagikia mtu, ulikuwa mwili wa kawaida, kwamba Kristo amekwisha kuja; na ni makosa, basi.

113 Biblia ilisema, Yesu atakapokuja, ya kwamba, "Kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri." Angekuwa . . . "Kuja kwake kutakuwa kama nuru itokayo mashariki hata magharibi, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri." Tunajua ya kwamba hiyo ni kweli.

114 Ndipo, tunapoona mambo hayo yakitukia, tunapoona mambo hayo yakitimia, basi tunajua ya kwamba kuna kundi la watu mchanganyiko ambalo limepanda pamoja na watu. Baada ya muda, kikundi kimoja kinakuwa juu zaidi upande mmoja, kingine kinakuwa juu zaidi upande mwingine. Na huo hapo

umati wako mchanganyiko. Hayo hapo majibu yako tena. Hapo unakuja.

115 Na ilipofanya hivyo, wakafika mahali pa Kadesh-barnea. Na walipofika Kadesh-barnea, hicho kilikuwa kiti cha hukumu ambapo majaribu hayana budi kutatuliwa.

116 Loo, laiti mngalilielewa, enyi kanisa dogo! Sasa hapa ndipo tunapotaka kubana kwa muda mfupi tu. Sasa sikiliza kwa makini. Kadesh-barnea ulikuwa wakati wa kujaribiwa. Na kila mtoto anayekuja kwa Mungu hana budi kujaribiwa. Hakuna ubaguzi, hata kidogo. Mungu hupima na kujaribu kila mtoto anayekuja Kwake. Je, hiyo ni kweli? Biblia ilisema wanajaribiwa. Na, kama, tunaona sasa wakati majaribio hayo yanapokuja, na majaribu.

117 Kuna nyakati za majaribu zinakuja kwa mataifa. Sasa, nasema hivi, mimi si mwanasiasa. Mungu huendesha taifa Lake mwenyewe. Yeye hayaendeshi mataifa haya; ibilisi anayaendesha haya. Kila mmoja wao, Biblia ilisema wanafanya hivyo. Ibilisi anaendesha kila taifa. Angalia wakati wa kujaribiwa unapokuja kwa mataifa.

118 Wakati wa kujaribiwa ulipofika kwa Israeli, ilishindwa. Na, iliposhindwa, Mungu aliikabidhi Babeli. Kama taifa, alishindwa.

Na wakati wa kujaribiwa kwa Roma ulipofika, ilishindwa.

Wakati wa majaribu ulipofika kwa Ugiriki, ilishindwa.

Wakati wa majaribu ulipofika kwa Ufaransa, ilishindwa.

Wakati wa kujaribiwa ulipofika kwa Urusi, ilishindwa.

119 Sikiliza. Nami nasema hivi kwa moyo wa uchaji kwa Mungu. Wakati wa kujaribiwa umefika kwa Marekani, nayo imeshindwa. Injili imehubiriwa kutoka mashariki hadi magharibi, kutoka kaskazini hadi kusini. Wamechambua kila mahali padogo, na ufa na kona. Miamsho mikubwa imetokea, ya Billy Graham na Jack Schuler, na ya Oral Robert. Na wanayo, loo, mamia tu yao, wamechambua kila ufa mdogo na kona. Ibilisi akatupa televisheni kule, na ndipo Mungu akaifanyia kazi kuwarusha watu kwenye televisheni; na kila mlevi katika chumba cha baa, au popote alipo, atasimama bila udhuru. Ndiyo, bwana. Wakati wa kujaribiwa umefika. Niliwaambia nini kutoka kwenye mimbara hii? "Mwaka jana, Marekani ilifanya kosa lake baya." Nikasema, "Kosa baya!" Hakika ilifanya.

120 Na tazama inachofanya sasa. Unaiona kwenye mambo ya kiserikali. Wanajaribu kwenda moja kwa moja na kuungana na Waarabu. Hivi hamjui? Neno la Mungu lilisema, "Yeyote anayewalaani Israeli atalaaniwa." Hakika.

121 Ninasimama na Israeli. "Wachukue ardhi yetu? Watachukua." Hakika.

122 Wanafanya vibaya. Hakika, wanafanya. Ndugu, tazama kila taifa lililogeuka dhidi ya Myahudi; walizama. Angalia—angalia Ujerumani ilipogeuka dhidi ya Myahudi, nao wakaiteketeza miili katika tanuru la kuchomea taka; basi angalia ni nini leo. Angalia Italia, iliyowageuka Wayahudi, wakati Mussolini alipowafukuza kutoka Italia; mtazame leo. Ikiwa hatukuwa tukiwalisha, wangekufa njaa.

123 Na hii hapa Injili imekuja na kutoa wito wa rehema kote katika mataifa, kwa miaka mingi, nasi tumeikataa. Na sasa anafanya kazi, ibilisi akiketi, anageuza mioyo ya watu hawa wa kisiasa dhidi ya Israeli, nao wanaunganika kule na Waarabu. Ndugu, karibu tumekwisha. Hiyo ni kweli. Tutazama, hakika kabisa.

124 Nalipenda taifa langu. Ninalipenda, kile linachosimamia. Lakini, ndugu, nampenda Bwana wangu zaidi ya kila kitu. Na ninapenda kuona taifa langu likipiga magoti, lakini ninaogopa hatutafanya hivyo kamwe. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Nini kilitukia? Umati mchanganyiko uliingia.

125 Angalia makanisa yetu, miaka michache iliyopita, walipokuwa na makanisa ya utakatifu ya mtindo wa kale, waliposimama kwa ajili ya Mungu na wenye haki, wakati wanawake walipovaa na kutenda kama mama wa heshima, wakati wanaume walipovaa na kutenda kama wanaume, watu walipoenda kanisani Jumapili asubuhi, walipokuwa na mikutano ya maombi ya usiku kucha, walipokuwa na aina ya kizamani. Walikuwa na uamsho halisi. Mungu alibariki. Aliondolea mbali kila adui mbele yao. Walikuwa wakiendelea na safari. Ila wakati kabari ya Akani ilipoingia kambini, bila chochote kilichosalia ila uharibifu. Tuko juu ya neno letu, Mungu . . . kwenye barabara yetu. Mungu hulitimiza Neno Lake.

126 Wakati wa kujaribiwa ulikuja. Wakati wa kujaribiwa ulikuja kwa kanisa la Kilutheri. Wakati wa kujaribiwa ulikuja kwa kanisa la Methodisti. Wakati wa kujaribiwa ulikuja kwa kanisa la Kipentekoste. Huja kwa kila kanisa. Huja kwa kila mtu. Wakati wa kujaribiwa.

127 Na kuna njia moja tu ambayo unaweza kujua kwamba uko sahihi: dumu na ramani ya Mungu ya Milele. Dumu na Neno. Kile Mungu asemacho, sema, "Hiyo ni kweli." Usichukue chochote pungufu au chochote zaidi. Kwa nini itulazimu kuwa na vibadala vya *hili, lile,* na *lingine,* wakati Neno la Mungu limejaa ahadi? Naam, bwana. Hatuhitaji kuchukua mbadala wowote. *Huu* ndio Ukweli. Mungu hulitimiza Neno Lake. Haidhuru linaweza kuonekana kuwa lisilo la kimantiki jinsi gani, Mungu hulitimiza Neno Lake, hata hivyo. Hakika alitimiza.

128 Je, babu yako angesema nini ikiwa baba ya babu yako angemwambia kwamba ungefika wakati magari yatapita

mitaani bila farasi? Angeweza kumcheka, labda. Lakini, yako hapa. Kweli.

129 Vipi kuhusu mambo haya mengine ambayo yangetokea, wakati unabii huu wote mkuu umetolewa? Lakini, tuko hapa.

130 Na siku moja Yesu atakuja, ile enzi tukufu ya Mwana wa Mungu. Aliahidi atalifanya. Aliahidi atahukumu dhambi. Ndugu, ama utakubali dhabihu iliyotolewa na Mungu kwa ajili ya dhambi, au utasimama peke yako katika Hukumu; taifa, kanisa, au mtu binafsi. Wakati wa kujaribiwa!

131 Angalia, walimtuma mtu fulani, kumi na wawili wao, kuona wangesema nini. Kumi kati yao walirudi, wakasema, "Loo, hatuwezi! Haiwezekani. Hatuwezi kabisa."

132 Lakini maskini Kalebu na Yoshua, walipanda juu ya kisiki, wakasema, "Tunaweza. Tunaweza."

133 Mbona? Inategemea kile unachoangalia. Ikiwa unatazama upande wa nje, "Je, inaonekana hivi? Je, inaonekana . . ." Usiangalie kile watu hao wanachosema, ama kile kitu kingine chochote kinachosema. Kama ni kinyume na Neno la Mungu, kaa na Neno.

134 Mungu aliwaahidi nchi hiyo. Hicho ndicho ambacho Kalebu na wao walikuwa wakiweka matumaini yao juu yake.

135 Soma Kitabu cha Kumbukumbu la Torati, uone jinsi Musa alivyowasahihisha. Kasema, "Nimefanya *hivi*, na nimefanya *vile*. Na Mungu akafanya *hivi*, na akasema *hivi*. Lakini hamngefanya." Mungu hudumu na ahadi yake.

136 Loo, wakati mwingine inaonekana kama ni ngumu. Sasa, nataka msikilize hili. Ni ngumu . . . Ni vita.

137 Huko chini Misri, Mungu alisema, "Nimewapa nchi hiyo, na vyote vilivyomo." Sasa, Yeye kamwe hakusema tu, "Nitawachukua, niwapeleke huko juu na kuwaketisha." Ilibidi wapiganie kila inchi ya ardhi waliyokuwa nayo.

138 Mungu, alipomwamuru Yoshua pale, alisema, "Uwe hodari na ushujaa mwingi; usiogope, wala usifadhaike: kwa kuwa Bwana Mungu wako yu pamoja nawe kila uendako."

139 "Bwana Mungu wako yu pamoja nawe kila uendako." Haijalishi ni nini, ni ngumu kiasi gani, kikwazo ni kikubwa vipi, hiyo haijalishi. Ikiwa ni chini katika bonde la uvuli wa mauti, "Bwana Mungu wako yu pamoja nawe kila uendako."

140 Loo, jinsi Yoshua angeweza kuwaita Israeli pamoja, kasema, "Simama hapa na utazame utukufu wa Mungu." Mungu yuko pamoja na Neno Lake. Mungu alitoa ahadi. Mungu akamwambia Yoshua, "Kila sehemu ambayo nyayo za mguu wako utakapokanyaga, hiyo ni yako. Nitakupa." Amina.

141 Kama ni kwa ajili ya wokovu, kama ni kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu, kama ni kwa ajili ya baraka zaidi, ikiwa

ni kwa ajili ya . . . ? . . . ikiwa ni kwa ajili ya kitu chochote ambacho Mungu aliahidi, weka alama za miguu! Amina. "Kila mahali patakapokanyagwa na nyayo za miguu yenu, nimewapa ninyi kuwa milki yenu." Mungu aliahidi jambo hilo. Mungu hutimiza Neno Lake. Neno la Mungu ni kweli milele. Ninaliamini. Unaliamini. Ndugu, ni wakati wa sisi kuweka alama za miguu. Hatuwezi kukaa papa hapa katika kambi hii hii. Moto unaendelea. Hebu tuendelee, kutoka utukufu hadi utukufu, kutoka kwa tukio la Biblia hadi tukio la Biblia. Hebu tufungue na kufungua mioyo yetu, tumwinulie Mungu mikono yetu. Dumisha akili timamu; kaa ndani ya Biblia. Usitoke nje ya Hiyo. Kaa papo Hapo.

142 Fuata! Tunaye Nabii wa Mungu; tunalo Neno la Mungu; na tunaye Malaika wa Mungu. Yeye ndiye anayeliongoza Kanisa hili kama vile tu alivyoliongoza katika siku hizo. Hiyo ni kweli kabisa. Neno la Mungu liko mbele yetu; Nabii wa Mungu ni Roho Mtakatifu; Malaika wa Mungu analiongoza Kanisa. Tunatembea katika Nguzo ya Moto, katika Utukufu wa Mungu, "Tumeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu." "Sasa sisi ni wana na binti za Mungu." Na ufunuo mkuu wa Neno, Roho Mtakatifu akilizamisha mioyoni, na kuzaa miti ya wokovu, maisha ya haki, upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, uvumilivu. Hakika ndivyo!

143 Haitatendeka tu kwa Maskani ya Branham, ama kwa maskani nyingine. Inatokea kwa watu binafsi. Kama Maskani yote ya Branham itakusanyika katika umoja huo, kitu chote kitakuwa kinakwenda katika kitengo kimoja kikubwa kwa ajili ya Mungu. Lakini kama kuna mmoja tu katika Maskani ya Branham anayetembea namna hiyo, Mungu ataenda pamoja na huyo.

144 Na njia moja tu ya kufanya jambo hilo, hiyo ni, kuambatana Nalo, endelea. Jina la Bwana libarikiwe! Mungu hulishika Neno Lake.

145 Mbona, wale jamaa walisema, "Hatuwezi kufanya hivyo. Hatuwezi kuwa na uamsho huko. Kila kitu kiko dhidi yetu. Loo, jamani! Waamori wako huko, na Wahiti, na wote. Wote wamezingirwa na ukuta. Nasi tunaonekana kama panzi."

146 Lakini maskini Yoshua, mwenye umri wa kama miaka arobaini, akijipiga kifuani. Naye Kalebu alikuwa akisema, Kalebu alikuwa amesimama pale, akisema. Kalebu akasema, "Unajua nini? Tunaweza hata na zaidi kufanya hivyo!" Loo, ndugu! Myahudi mdogo, mwenye pua iliyopinda amesimama pale, akiruka-ruka, akisema, "Tunaweza hata na zaidi! Si kwamba tu tunaweza, bali tunaweza hata na zaidi!" Kwa nini? Mungu alisema hivyo! [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili.] Hilo latosha.

147 Ndugu, tunaweza kuwa na uponyaji. Tunaweza kuwa na miujiza. Tunaweza kuwa na uamsho. Tunaweza kuwa na baraka. Kwa nini? Mungu alisema hivyo! Tunaweza kuwa na pentekoste ya kweli. Tunaweza kuwa na uamsho wa kweli. Mungu alisema hivyo! Mungu hutimiza ahadi Yake.

148 Kama vile Mungu hutimiza ahadi Yake kwa baraka Zake, Mungu hutimiza ahadi Yake kwa hukumu Yake. Hatuna budi kuchukua hukumu au baraka. Hatuna budi kusonga mbele au kurudi nyuma. Hatuna budi kwenda pamoja Naye, ama twende peke yetu. Hakuna anayeweza kwenda nayo huko. Dumu kwenye Neno Lake.

149 Ninaweza kumkumbuka rafiki yangu mzuri sana, ambaye ameenda Utukufuni; loo, ndugu mzee aliyebarikiwa, mtu mtakatifu, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, kwa jina Paul Rader. Wakati mmoja, huko nje kwenye Pwani ya Magharibi, wakati kabla tu hajafa, mnajua ushuhuda wake. Wimbo wake ambao ameuandika, *Amini Tu,* ndio ulioniita mimbarani. Sijui kama Paul, kule Utukufuni, anasikia wimbo huo wa kale ukiimbwa na maelfu na maelfu, na kwa lugha tofauti. Alijuaje ya kwamba maskini mvulana huyo mdogo aliyeketi mbele yake pale, amevaa viatu chakavu, na hakuna hata tai ya shingo, akihitaji kukatwa nywele, kwamba Mungu angeniruhusu niupeleke wimbo huo kote ulimwenguni! Mungu hulitimiza Neno Lake.

150 "Mimi, Bwana, nimeipanda; nitaimwagilia maji mchana na usiku," Akasema, "wengine wasije wakaipokonya kutoka mkononi Mwangu."

151 Inaweza kuonekana kama inazama, lakini haitazama kamwe. Loo, ile meli ndogo ya zamani usiku ule, wakati matumaini yote yalipokwisha, naye akatupwa huku na huku, ilionekana kana kwamba saa ya mwisho ilikuwa imewadia. Lakini, mara moja, Mtu fulani akaja akitembea juu ya maji, akiwa mtulivu tu. Yeye yuko kila wakati. Hachelewi kamwe. Mwatuko mmoja zaidi na meli ingezama. Lakini Yeye yuko kila wakati. Hakika.

152 Siku hiyo, kule Babeli, wakati watoto wa Kiebrania walipoingia kwenye ile tanuru ya moto, ilionekana kana kwamba mwisho ulikuwa umewadia. Lakini walipoingia, "kulikuwa na Mmoja kama Mwana wa Mungu," aliyesimama karibu nao. Yeye yuko kila wakati. Hachelewi kamwe. Yeye hulitimiza Neno Lake. "Nitakuwa pamoja na wewe."

153 "Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya," alisema Daudi. Yeye yuko kila wakati.

154 Yeye hutimiza ahadi Yake. Yeye ni wa Milele, Kweli. Hawezi kushindwa. Neno Lake haliwezi kushindwa kamwe. "Mbingu na nchi zitapita, lakini Maneno Yangu hayawezi kupita kamwe."

155 Paul alisema, wakati mmoja, alikuwa na ma—mapambano. Alikuwa nje visiwani na alikuwa na homa. Alikuwa karibu

maili mia moja kutoka kwa daktari. Huko nje kwenye vinamasi, na kinamasi, homa ya maji meusi ilikuwa imemshika; na hicho ni kifo mara moja. Na ikawa giza. Naye akamwambia maskini mke wake, mwaminifu, akasema, "Wewe simama karibu nami, mpenzi, na uombe. Kunakuwa giza sana chumbani, lakini," kasema, "Ninamwamini Mungu. Na sijali kinachotokea. Ninamwamini Mungu. Nitakaa nayo moja kwa moja." Kasema, "Wewe kaa hapa na uombe, mpenzi." Naye akaomba. Na ikawa giza zaidi, akasema, "Mpenzi, inakuwa giza zaidi kwenye chumba. Lakini, loo, ninajihisi mwenye amani."

156 Na baada ya kitambo kidogo, giza likaingia, akatoka nje. Akaingia katika ndoto. Alidhani alikuwa anaota. Alikuwa huko Oregon, alikotoka, akikata mbao. Na bosi akasema, "Paul, nenda juu ya mlima pale, na unikatie mti, inchi *kadha*, urefu wa futi *kadha*, na uniletee kwangu."

Akasema, "Sawa, bosi. Nitafanya hivyo."

157 Akapanda juu pale, na kuangusha maskini mti wake wa kale, na kulichoma shoka, akanyoosha mkono kuushika, na hakuweza tu kuuinua juu. Alininii tu. . . Alisema, "Nimepoteza nguvu zangu. Siwezi kwenda zaidi. Nimepoteza nguvu zangu. Mbona," akasema, "mimi hapa, mtu mkubwa. Nina uzito wa zaidi ya pauni mia mbili. Nina mgongo mkubwa, wenye misuli. Mbona," akasema, "Nilikuwa nikipiga magoti pamoja, kushika gogo la saizi yoyote, na ningeweza kuliinua ili waweke minyororo chini yake." Akasema, "Na hapa, kwamba mimi. . . kiungo kidogo, si kikubwa kuliko *hicho,* na sikuweza kukiinua." Akasema, "Nilijitahidi na kujaribu, mpaka nguvu zangu zote zikaisha. Loo," akasema. "Kisha nikawaza, 'Ninaweza kufanya nini?'" Akasema, "Nilikaa chini na kuegemea kwenye mti." Akasema, "Loo, nina huzuni sana. Bosi wangu anautaka maskini mti huu kule chini, na mimi si mwanaume wa kutosha kuushusha."

158 Loo, kile Bosi wetu anachotaka! Anataka Kanisa lisilo na doa, lisilo na kunyanzi. Anataka kundi la watu waliooshwa kwa Damu. Anataka watu wenye imani, watakaosimama juu ya Neno Lake na kusema, "Hiyo ndiyo Kweli ya Milele ya Mungu. Ilikusudiwa mimi, nami ninaiamini."

159 Akasema, alipokuwa ameketi pale, alikuwa ameegemea kwenye mti, na alikuwa analia. Na akasema alimsikia bosi wake akizungumza, na kusema, "Paul?"

160 Naye akasema, "Naam, bosi, mimi hapa. Lakini nimepoteza nguvu zangu zote. Siwezi kwenda mbali zaidi. Nimejaribu kufanya, na nimejaribu kukutii na kufanya ulichosema nifanye, lakini siwezi tu kukiondoa kitu hiki kutoka chini." Akasema, "Nimejitahidi. Nimejaribu. Nimefanya kila kitu."

161 Nami nashangaa tu kama huo sio mtazamo wa wahubiri wengi wazuri wenye moyo wa kweli siku hizi, ambao wametamani kuona Kanisa likijengwa bila doa wala kunyanzi,

kuona ahadi za Mungu zikidhihirishwa. Tumezozana na kujaribu, na kupiga mayowe na kulia, na kuhubiri mpaka tukapwelewa na sauti, na kulalia mito yetu na kulia. “Ee Mungu, kwa nini, tunaponyoshwa tu, ndipo shetani anaingia, na kupasua na kurarua, anaangusha tu kila kitu tulicho nacho? Tunaweza kufanya nini tunapowaona watu wetu wapendwa, na jinsi walivyotawanyika na kwenda huku na huko namna hiyo?”

162 Kisha akasema, aliposikia sauti yake, ya bosi wake, akawaza, “Hiyo inasikika kuwa ya ajabu. Sijawahi kusikia sauti yangu ikinena . . . huyo bosi akiongea nami kwa upole hivyo.”

163 Ndipo akasema, “Nilipogeuka, alikuwa ni Bosi wangu halisi. Ilikuwa ni Bwana wangu, Mwokozi wangu.”

164 Alisema, “Paul, unajisumbua hadi kufa. Hiyo haitakufaa chochote.” Akasema, “Paul, huoni kile kijito kidogo cha maji kinachotiririka pale?”

Akasema, “Naam.”

165 Akasema, “Ingiza tu kitu hicho ndani. Panda juu yake na ukipande kuteremka chini hadi kambini. Kinakwenda kambini.”

166 Akasema, “Niliruka na kulibiringisha lile gogo, na kulirukia lile gogo. Nilishuka juu ya maporomoko, nikipiga mayowe kwa sauti yangu yote, nikipiga mayowe, ‘Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake!’”

167 Na alipojirudia, alikuwa moja kwa moja huko katikati ya sakafu. Na mkewe akipiga kelele kwa sauti yake yote. Alikuwa nje katikati ya sakafu, akisema, “Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake!”

168 Na, ndugu, dada, najua majaribu ni magumu. Ninazeeka, na nimehubiri. Nimefanya kila kitu ninachojua kufanya. Nimefikia mahali, ambapo naona siwezi kufanya zaidi. Nimeweka tu kitu chote mkononi mwa Bwana Yesu, nami nimekipanda. Nimepanda juu ya ahadi ya Mungu, “Mimi, Bwana, nimeipanda. Ninainyunyizia maji, mchana na usiku, ili wengine wasiweze kuinyakua kutoka mkononi Mwangu.” Kanisa la Mungu litadumu milele.

169 Neno la Mungu litasimama, sawa kabisa, milele. Na haidhuru kama falme zikija, ama mabomu ya atomiki yakianguka, ama Marekani ikirudi nyuma, lolote litakalotukia, *Hili* ni Neno Lake. Analitunza. Nami nimepanda juu Yake. Ninaliamini kwa moyo wangu wote.

Na tuombe.

170 Yesu mbarikiwa, loo, ni safari iliyoje! Chini juu ya mawimbi ya furaha, chini kupitia mkondo wa haleluya, loo, nimelipanda tu! Uliahidi. Ahadi zako zote ni za kweli. Na tunajua ya kwamba kila moja yazo inashuhudia kwamba ni za kweli. Na kote katika

nyakati, tumeona Biblia ya zamani iliyobarikiwa ikifunuliwa kwetu, na sasa ile saa kuu inakaribia, saa ya usiku wa manane.

171 Bwana, wahudumu wakuu, watakatifu, wa Injili, wamezunguka taifa, wakihubiri, wakilia, wakinywa maji ya matawi, wakiteswa, kukimbia kutoka nguzo hadi nyingine, kukimbia miji, kufungiwa, kudhihakiwa, kudharauliwa, kuchekwa, njaa.

172 Lakini, Kanisa limeendelea moja kwa moja, kwa maana Neno Lako lilisema, "Juu ya mwamba huu, nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda kamwe." Nasi tumepanda juu yake, leo, ule Mwamba, Ukweli wa Milele wa Mungu, uliofunuliwa wa Bwana Yesu Kristo. Juu ya Mwamba huo imara, Kanisa limesimama leo. Wakana Mungu, wakomunisti, nguvu za asili za dunia hii, zimeinuka, na zimepiga na zimevamia. Lakini, amejengwa juu ya Mwamba huo imara.

173 Ibilisi ametuma—ametuma watafuta makosa. Imedhihakiwa. Inateswa. Inaitwa kila kitu, katika ulimwengu. Nasi tumegongwa huku na huku, na kupimwa na kujaribiwa, na, loo, kila kitu. Lakini, Ee Mungu, kama Kalebu na Yoshua wa kale, tungali tunasema tunasimama Milele kwenye Neno la Mungu. Yeye hutimiza ahadi Yake. Alisema atafanya hivyo, nasi tunaamini.

174 Na jalia kila mtu hapa asubuhi ya leo, apate mtazamo wa karibu wa jambo hilo sasa, kile linachomaanisha, kwamba sasa—sasa tumelipanda Hili. Siku moja tutakuwa kwenye kambi, ambapo watakatifu wamepiga kambi katika upana wa dunia. Mungu na watoto Wake watakuwa wakifurahi, milele. Tujalie, Bwana.

175 Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, macho yetu yamefumbwa, katika maskani hii asubuhi ya leo. Sijui kama, katika Jina la Kristo, kama mtu angekuwa na ujasiri wa kusema, "Ndugu Branham, leo hii, sasa hivi, katika kanisa hili, sasa ninamwinulia Kristo mikono yangu, na kusema, 'Kuanzia leo, na kuendelea, nitapanda juu ya Neno Lako, Bwana.' Nitasimama hapo, nimkubali Kristo kama Mwokozi wangu; nisijaribu kamwe kufanya mambo ili kujaribu kustahili wokovu wangu mwenyewe. Nitamwamini tu Bwana Yesu na kumkubali Yeye. Naye aweke huo upendo wa kilindi wa Kiungu ndani ya moyo wangu, na amani ipitayo akili zote. Nitamngojea Roho Mtakatifu anipe. . .Nilisimama, wakati mmoja, na nikafikiri ningeweza kwenda kufanya jambo hilo, lakini nikagundua ya kwamba singeweza." Hakika, hutawahi. Lakini, kama utakaa tu hapo muda mrefu wa kutosha, mpaka Yeye atakapofanya jambo hilo, basi litakaa hapo, basi limetiwa nanga.

176 Lakini ukijaribu tu kufanya hivyo, utashindwa, na huna budi kushindwa. Hiyo ndiyo sababu una mema na mabaya yako, na kuingia-na-kutoka, na mambo yote unayofanya. Ni

kwa sababu unajaribu kuifanya. Unasema, "Loo, ninaamini niko sawa sasa." Hiyo siyo. Hiyo si—hiyo siyo. La. Ni Roho Mtakatifu anayeingia. Anachukua mahali hapo. Anaondoa mizizi yote ya kale ya uchungu, hasira ya kale, na hamaki, na wivu, na kupenda ulimwengu na kadhalika. Huondoa yote kutoka kwako, na kisha wewe ni kiumbe kipya.

177 Waweza kuinua mkono wako, useme, "Kristo, nifanye Mkristo wa aina hiyo, asubuhi ya leo." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, mama. Na Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada. "Nifanye Mkristo wa aina hiyo, asubuhi ya leo. Nataka kuwa kama Yesu. Nataka mizizi yote ya uchungu iondolewe moyoni mwangu."

178 Sasa, kumekuwa na wengi wenu mlioinua mkono wenu. Sasa, papo hapo ulipo, ukipenda, kwa moyo wako wote sasa, siyo—siyo tu kufikiria, lakini amini ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, amesimama moja kwa moja karibu nawe, na atakuondolea huo uchungu wa kale, hiyo itakufanya kile unachotamani kuwa, atafanya hivyo papo hapo ulipo... Atakufanyia upasuaji katika hospitali *yako*, kama utamruhusu tu afanye hivyo.

> Kwa maana mambo yote yawezekana, amini tu.
>
> Amini tu, amini tu,
> Mambo yote yawezekana, amini tu;
> Amini tu...

179 Endelea tu kuomba. Bwana...Kumbuka, mtoto, ni nafsi yako. Huenda usiwe katika ibada nyingine, hata kidogo. Huenda ikawa hii ndiyo ya mwisho. Acha Mungu afanye sasa hivi.

180 Sema, "Ndugu Branham, je, nije madhababuni?" Ikiwa unataka, hakika. Ikiwa hutaki, kaa papo hapo ulipo.

181 Wewe amini tu. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ndivyo ilivyo.

182 Kama ungependa kuja madhabahuni na kuomba, iko wazi. Ukitaka kubaki ulipo, na kuomba; ni nafsi yako, ni, wewe ndiwe.

183 Wakati umekaribia, ndugu. Kanisa karibu limekamilika. Kijito cha zamani kina matope. Tumevuta juya na kuvua samaki, na kutupa maskini hizi chubwi huko mpaka kitu hicho chote kimejaa matope. Nguruwe wengi sana matopeni. Amejaa matope.

184 Kama mimi, mhudumu, ninahisi tu hili, ya kwamba, kama Mungu atafanya jambo hilo, lazima itamhitaji Mungu. Siwezi. Kwa hiyo, ni juu yako. Hilo hapo Neno, hiyo hapo Kweli, unaiona ikifunuliwa papa hapa mbele yako. Mwisho umekaribia. Yesu anaweza kuja wakati wowote. Huenda hata kusiweko na

Marekani yoyote, wakati jua linapotua usiku wa leo. Wangeweza kutuma mabomu elfu tano ya atomiki kwa wakati mmoja; hakungekuwa hata na kiumbe kimoja hai duniani, katika saa nyingine kuanzia sasa. Ukitaka . . . Sasa ni juu yako.

Wazia jambo hilo sasa tunapoomba.

185 Mbarikiwa Baba wa Mbinguni, kwenye kufungwa kwa Neno hili, ninapozifungua kurasa, Ujumbe umetiwa muhuri sasa. Kuja kwa Bwana kunakaribia. Watu kadhaa humu jengoni, asubuhi ya leo, waliinua mikono yao na kusema, kwa hilo, "Nataka kuwa Mkristo. Ninataka kuwa mtumishi halisi wa Mungu, aliyezaliwa mara ya pili."

186 Bwana, labda miaka mingi, umeshughulika na mioyo yao. Wewe—Wewe umewaambia hivyo. Neema yako bado imewafikia. Hawajaenda kabisa, bado. Wengine wameenda mahali, hawana shauku tena. Mwaka mmoja uliopita, walikuwa wakiinua mikono yao, wakisema, "Vema, ningetaka kuwa Mkristo." Sasa imeenda mbali sana; hawajisikii hivyo tena sasa.

187 Karibu kote! Na hilo linaonekana kuwa ndio mwendo wa jumla wa taifa, kuwasikia wainjilisti mashuhuri, wanapovuka mataifa. Wametuma vipapasio. Wamefanya kila kitu. Wameunda vikundi. Wanatembelea nyumba, kwa wale ambao wangeinua mikono yao na kujaribu. Ambapo maelfu na maelfu walianza, wawili au watatu wangeshikilia. Vema, imekwisha, Bwana. Imekwisha, Mungu. Tumekwisha.

188 Ee Baba, najua ya kuwa Wewe ulisema, ya kwamba, "Wote waliokuwa wamemjia Kristo, ungewahifadhi." Na ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Nami naamini, Bwana, ya kwamba utawahifadhi wale ambao mioyo yao na akili zao zimekaa Kwako. Nami nakushukuru, Bwana, kwa ajili ya Kanisa, na kwa ajili ya watakatifu wa Mungu aliye hai walio katika Kanisa hilo, Mwili huu mkuu wa kiroho!

189 Lakini, Ee Mungu, jinsi moyo wangu unavyotetemeka kwa ajili ya wale walio nje ya Hilo, nikijua ya kwamba wanaona maandishi ya mkono ukutani, kuona mambo makuu yakifanyika, vibao vya kuelekeza. Nayo Marekani bado imejaa vichekesho vichafu vya zamani, na vipindi visivyokaguliwa kwenye televisheni, redio, na hadithi za mapenzi, na wenye dhihaka na wenye kucheka, na watani wakubwa, na uinjilisti wa Hollywood.

190 Na, Ee Mungu, ni—ni saa ya usiku wa manane inagonga, kweli. Yuko tayari kwenda. Basi nifanye nini, Bwana? Nimekuwa na wasiwasi; nimelia; nimeomba. Mimi—mimi . . . Ni juu Yako tu sasa, Bwana. Mimi—mimi . . . Hayo ndiyo yote ninayoweza kufanya. Nimeihubiri. Nitasimama tu juu ya Neno moja kwa moja, Bwana. Ninajaribu kupanda hadi kambini sasa. Muda hautakuwa mrefu.

191 Sasa, Mungu, kwa wale walio na moyo wa uaminifu leo hii. Mungu, wafanyie jambo fulani sasa hivi. Wajalie wawe watoto Wako, kuanzia siku hii na kuendelea.

192 Waponye wagonjwa katikati yetu, Bwana. Wape afya njema. Warudishe wale waliorudi nyuma baridi, Bwana. Wafanye wajue kwamba wao tu ni . . . Wanacheza kwenye uwanja wenye hatari kabisa. Hivi karibuni watakuwa wameondoka, itakuwa imechelewa kupita kiasi basi. Jalia sasa kwamba Roho Wako atatushughulikia pakubwa. Katika Jina la Kristo. Amina.

193 Kwa vijana, ningesema hivi. Kama ningeweza . . . Asubuhi ya leo, baada ya siku ya kuzaliwa jana, ya miaka arobaini na minane katika maisha haya. Miaka ishirini na kitu ya hiyo, yapata miaka ishirini na minne, nimetumia kwa ajili ya Bwana Yesu. Nikiwa mvulana wa kama miaka ishirini na mitatu, ni—nilianza kuhubiri Injili.

194 Ikiwa kuna majuto yoyote niliyo nayo, majuto yoyote; kama ningeweza kugusa kitufe, asubuhi ya leo, na kurudi kwenye u—umri mzuri wa miaka kumi na sita au kumi na saba, ningetaka tu kufanya hivyo kwa jambo moja, yaani, kumtumikia Kristo. Hiyo ndiyo inayomaanisha, kumtumikia Kristo peke yake. Mungu Ambaye anaujua moyo wangu, anajua hiyo ni kweli. Mtumikie Kristo, peke yake.

195 Sijawahi kuona chochote, wala kufikiria chochote, ambacho kimewahi kulinganishwa na nanga hii iliyobarikiwa ya Kristo moyoni mwangu. Sijui chochote. Nimesafiri baharini. Nimeruka angani. Nimeona tamasha zote ulimwengu ulizo nazo. Nimeona maajabu saba ya ulimwengu, nimeona mambo saba mashuhuri, hasa, ya ulimwengu. Nimeona pande zote za milima, karibu sana, za dunia. Nime . . . Mimi ni mwindaji; nimewinda katika namna zote za mataifa. Nimefanya kila kitu; nimevua samaki. Nimepanda farasi. Nimefuga. Nimefanya kila kitu nilichojua kufanya. Nami nitasema hivi, kwamba kuna, yote yakiwekwa pamoja, hayatafanya nukta moja ndogo, kwa upendo wa Bwana Yesu Kristo.

196 Ningefanya nini? Nini kingeweza . . . Loo, naam, hiyo ni hawa watoto wadogo hapa. Nimekuwa na maskini marafiki zangu wasichana, na kulainisha nywele zangu chini. Na kurudisha kioo changu kwenye gari langu, na kutoka na miadi yangu. Nilifikiri . . . Lakini haikuridhisha hata hivyo. Kuna kitu unachokosa, kila wakati.

197 Nimemwona msichana mwenye macho mazuri ya kahawia, na ingekuwa . . . Mnajua jinsi ungejisikia, kama vijana. Nilidhani ni hivyo tu. “Kama ningeweza tu kuwa na miadi na msichana huyu, ingeninii tu . . . inge—ingeondoa tu wasiwasi wangu wote. Hilo, hilo lingetosheleza kabisa.” Ningekuwa na miadi naye, na kuwa naye nje, dakika kumi na tano, na kutafuta mtu mwingine. Kamwe hairidhishi. Loo, hakuna kitu.

198 Lakini, saa hiyo yenye baraka! Jina Lake lihimidiwe! Chini katika kibanda cha kale cha makaa, nyuma ya jengo, nikipiga magoti kwenye gunia kuukuu la nyasi, kwenye uchochoro, ambapo nilipiga magoti pale kwenye ardhi yenye unyevunyevu, na kusema, “Bwana Yesu, unaweza kunifanyia jambo?” Hapo ndipo amani ipitayo ufahamu wote, miaka ishirini na minne iliyopita, ilipotia nanga hapa katika moyo wangu huu. Na inastahili yote yaliyopo ulimwenguni kote. Sijawahi kuona kitu cha kulinganisha nayo.

Kupitia hatari nyingi, taabu na mitego,
Nimekuja tayari;
Neema ndiyo iliyonileta salama umbali huu,
Ni neema ambayo itanipeleka.

199 Nilimtumaini katika saa za ugonjwa na ajali. Nimemtumaini wakati ndege zilipokuwa zikizunguka kwenye dhoruba, na hamkujua ni nini. Nilisema, “Bwana Yesu, umemalizana nami? Ikiwa sivyo, nyoosha ndege hii.” Na kuiona ikilainika, kwa hali yake inayofaa.

200 Nimesimama kwenye kliniki ambapo madaktari bora katika mataifa, kwenye. . .Nao wangenitazama na kusema, “Dakika zingine chache tu za kuishi; anaenda.” Na wakati madaktari bora ambao wangeweza kupatikana kwa ajili yangu.

201 Nami nikasema, “Bwana Yesu, umemaliza nami?” Na kwa ghafla, nilikuwa nimejirudia. Hakika.

202 Loo, neema ya ajabu, jinsi sauti hiyo inavyosikika tamu! Jinsi natamani ningekuwa na lugha kuelezea ni nini. Ni kubwa sana kwa akili ya mwanadamu. Chukua neno langu. Usichukue kibadala, rafiki. Usichukue kibadala. Usiende tu na kusema, “Vema, sasa, mimi hufanya *hivi*. Ni—ninakuambia nini, mimi ni mtu mzuri sana.” Usitegemee hilo. Usifanye hivyo. Kaa tu hapo mpaka Kitu fulani kifikie tu, kiondoe dhambi yote, na kuweka busu pale ambalo linawaka tu. Na wakati majaribu yanapokuja, huna haja ya kujiuliza kama nitafanya hivyo, ni Kitu fulani tu kinachoshikilia pale.

203 Na kama mtu mwenye umri wa makamo sasa, sina budi kushuka na kufikiria jambo hili, kwamba moja ya siku hizi sina budi kuondoka. Yesu akikawia, sina budi kwenda. Sijui itakuwaje nitakapofika mwisho wa safari. Sijui. Sitegemei mahubiri yangu. La, bwana. Hapana, sitegemei mambo ambayo nimefanya. Ee Mungu, hapana. Loo, hilo na liwe mbali nami. Nimefanya mambo, tangu nimekuwa mhubiri, nilipuuza na kufanya *hili* na *lile*. Sitaki kuamini chochote, hicho. Hapana, bwana. Sitaki kusema, “Bwana, nimekuletea zaidi ya watu milioni moja.” Hiyo haina uhusiano wowote nayo; si kitu. Kitu pekee ninachotumainia, ni neema Yake, ahadi Yake, Neno Lake.

204 Bwana, umesema. . .Nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya. Ulisema, “Sitakuacha kamwe wala

sitakupungukia." Ninapouminya mto huo, na jasho baridi la mauti linatoka kwenye paji la uso wangu, Yeye atakuwapo. Kwa hakika kama vile ninavyosimama hapa, Yeye atakuwapo.

205 Nitakapohubiri mahubiri yangu ya mwisho, nifunge Biblia na kuondoka mara ya mwisho, kazi imeisha; Yeye atakuwepo. Naam, bwana. Na kwa hakika kama ninavyoamini ya kwamba Yeye Yuaja; atakapokuja tena, nitakuwapo, pia. Naam, bwana. Sio kwa sababu ninastahili. Ni kwa sababu Yeye amefanya, kwa ajili yangu. Nami ninaikubali juu ya msingi wa Neno Lake la Milele. Nami ninajua, kwa hilo, kulikuwa na jambo fulani lililotukia. Jambo fulani lilitukia. Si kwamba ninaweza kupiga kelele kiasi gani, jinsi ninavyoweza kusema vizuri. Kama ningekuwa ndiye mhubiri mashuhuri kuliko wote ulimwenguni, kama ningaliwafufua wafu, chochote kile, hilo halina uhusiano wowote nalo. Ni kwa sababu jambo fulani lilitokea. Kitu kilifanyika *hapa* ndani. Iliondoa wivu wote wa kale, na uchungu, na uovu, na kila kitu, kutoka moyoni mwangu. Na sasa ninampenda tu, mchana na usiku. Kitu kilitokea. Ninataka kumwona, siku moja. Nakutaka wewe, vile vile, pia.

206 Kanisa dogo, linalojitahidi sasa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kamwe msiyumbayumbe katika siku hii. Ukiyumbayumba, tubu upesi, ruka urudi moja kwa moja. Unaona? Ukijikwaa kidole chako, usianguke. Ukianguka, inuka. Simama. Jamani! Simama. Hakika.

207 Ikiwa umekosea. Sasa, katika uamsho huu unaokuja... Ulirudi tu nyuma na ukawa baridi, kutojali. Amka, shuka kwenye Biblia yako. Nenda nje kwenye bustani ya tofaa mahali fulani. Ondoka uwe peke yako, na useme, "Mungu, sasa niko hapa. Samahani kwa jambo hili."

208 Utapata kichapo kwa ajili yake, kumbuka hilo tu. Ndiyo, kwa kweli. Utavuna ulichopanda. Ndiyo, bwana. Lakini, chochote unachofanya, chukua kichapo chako hapa. Inuka moja kwa moja na unyooke, na useme, "Baba, mimi hapa. Nicharaze vile unavyoona inafaa, Bwana. Mimi hapa." Hiyo ni kweli. Kisha urudi moja kwa moja, na "haleluya" moyoni mwako. Mungu akiachilia kichapo kukushukia, sema tu, "Ndiyo, Bwana. Ninastahili kila sehemu yake." Endelea tu. Mungu atakupitisha, sawa. Itakwisha, moja ya siku hizi.

209 Nafikiri ule wimbo mzuri wa zamani Ndugu Neville na hao walikuwa wakiimba, "Hivi karibuni nitamaliza, shida na majaribu." Naam, hiyo ni kweli.

210 Ni wangapi wanampenda? Hebu tuone mikono yenu? Vema. Tupe sauti, *Neema Ya Ajabu*. Kila mtu akae kimya, kwa dakika moja. Polepole sasa.

> Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika ni tamu,
> Iliyomwokoa mwovu kama mimi!

Nilikuwa nimepotea wakati mmoja, lakini sasa nimepatikana,
Nilikuwa kipofu, bali sasa ninaona.

Ilikuwa ni neema ambayo ilifundisha moyo wangu kuogopa,
Nayo neema ikaniondolea hofu zangu;
Jinsi hiyo neema ilivyoonekana ni ya thamani
Ile saa niliyoamini!

Sasa sisi sote, pamoja.

Tukishakuwa huko miaka elfu kumi,
Niking'aa sana kama jua;
Hatuna siku chache za kuimba sifa za Mungu
Kuliko tulipoanza mara ya kwanza.

211 Nilikuwa nikimsikia mzee Doc Davis, wengi wao, na nimewasikia wengi wa watakatifu wa kale, walipokuwa wakishuka, baada ya kupanda, na huduma ilikuwa inaiva. Nimewasikia wakizungumza kuhusu walivyohisi. Anza tu kutambua hilo sasa. Amina. Anza tu kulitambua. Loo, jinsi gani, ni jambo la ajabu jinsi gani!

212 Ningeshikilia nini leo? Ningeenda wapi? Unaenda wapi? Amina. Ningefanya nini? Wapi? Je, nini kingenipata leo kama si Kristo? Matumaini yangu yangetiwa nanga wapi? Ningekuwa mwendawazimu. Ninapoona yale yanayokaribia kutukia, na kujua hayo yalikuwa ndiyo yote, milele, loo, jamani, ningefanya nini?

213 Lakini, loo, nina furaha sana. Nina furaha sana. Ni mapambazuko tu ya siku. Tuko kwenye ndoto tu. Tunajiandaa kuamka. Loo, katika ndoto mbaya, tuseme; kutoka kwake, kuingia kwenye majira ya kuchipua; ujana wa milele, afya ya milele, furaha ya milele, amani ya milele. Je, si ni ajabu? Yeye ni wa halisi sana!

214 Sijui ni wangapi hapa ni wagonjwa sasa, na wanataka kuombewa? Hebu tuone mikono yenu. Vema.

215 Ningependa kuwaambieni kilichotokea wiki hii iliyopita. Tumekuwa na baadhi ya mambo ya ajabu sana kutokea katika mkutano, bila shaka, kwenye jukwaa. Na nimekuja kwenye m—mfano wa kitu fulani, ambacho kinaonekana tu kuwa kikubwa zaidi kuliko kile kilichokuwa.

216 Nimekuja jukwaani, na Mungu ametoa kipawa cha ka—karama ya kinabii, ambayo inaweza. . .Hilo halina tashwishi. Ninaweza kukuthibitishia hilo, papa hapa. Unaona? Hilo halina tashwishi. Lakini naona haifanyi kazi jinsi inavyopaswa, kwa sababu ni kipawa tu. Jambo lingine, ni mtu binafsi, unaona. Inahusu mtu binafsi, kupitia kipawa.

217 Lakini nilifanya jambo fulani hivi majuzi, nilijaribu kuwapata watu kule Oakland, kufikia tu ambapo. . .kwenye

uwanja mkubwa huko. Nikasema, "Uwepo Wake tu," na kudumu tu moja kwa moja na Neno hilo. Na kuwapata watu na . . . Unajua nini? Kulikuwa na uponyaji zaidi ya ninaoamini nimewahi kuona katika mkutano wowote ukifanyika, nje ya mikutano mikubwa kama huko Afrika na kote namna hiyo, lakini kwa ukubwa wake. Watu wakitambua tu Uwepo wa Mungu, katika mkutano, wameketi tu pale na kuingia katika Uwepo wa Mungu. Nao watu wangeinuka, wameponywa; macho yenye makengeza, yamenyooka. Na, loo, ni . . .

218 Naamini inafika wakati ambapo . . . Paulo alisema, "Palipo na unabii, utabatilika; palipo na lugha, zitakoma." Ninaamini inafika wakati ambapo watakatifu watakusanyika hivi, na roho ya upendo tu itasambaa kwa watazamaji. Na kabisa, kila mtu humo ndani, yote ambayo ni mabaya yataondolewa. Utakuwa ni Uwepo mkuu sana wa Roho Mtakatifu.

219 Ninaamini, tunapopaswa kuwawekea mikono na kuwaombea sasa, ni kuwasiliana labda kwa mhudumu aliyetiwa mafuta, na kuwekewa mikono, kama tu baraka kwa Mungu. Lakini ninaamini inakuja wakati ambapo Kanisa la Mungu litaitwa litoke, namna hiyo, ambapo watakatifu wataketi pamoja, na Roho Mtakatifu ataingia tu, ashawishi tu, kama tu ilivyokuwa kwenye Siku ya Pentekoste. Unaona? Na kuwaponya tu watu, na kuwainua watu, na mambo makuu. Ninaanza kuona ikitokea.

Kwa sababu, nakuambia kwa nini.

220 Watu wametoka na karama, hiyo ni kweli. Sina shaka kusema. Mimi si mkosoaji wa mtu yeyote. Wanachoamini, hiyo ni juu yao, unaona. Lakini, nimeona watu wenye huduma zenye karama, lakini walienda na, kwa namna fulani wakafanya ninii—ninii . . . Ningesema nini? Sasa, kwa heshima na kwa upendo, na Mungu anajua inatoka moyoni mwangu. Unaona? Kwamba wamefanya zaidi kama ja—jambo la kukusanya pesa kutoka kwake, unaona, wakusanye tu watu na kutaka kujiwekelea jambo fulani kubwa mno. Na labda wanatoa pesa, na, vema, hiyo inaweza kuwa sawa. Lakini inaonekana kwangu mimi . . .

221 Wanasema, "Vema, mwisho unakuja, watu wanahitaji nini na pesa zao?" Vema, *wewe* unahitaji nini nayo, wewe mwenyewe? Unaona?

222 Kwa hivyo, ja—jambo ni kwamba, ni kuwafikishia tu watu Injili, unaona, ni kuhubiri. Ninaamini ikiwa tu . . .

223 Na karama, unaona, ishara. Na, sasa, mtu angeweza kuja hapa, asubuhi ya leo, na kusimama hapa kwenye mimbara hii, na kufanya miujiza mikubwa na ishara. Hiyo hata haingemaanisha kuwa mtu huyo ameokoka. Mashetani hufanya ishara na maajabu. Hakika, wanafanya hivyo. Hakika, wanafanya hivyo. Na Biblia ilisema wangefanya zaidi ya hayo, katika siku

ya mwisho. Vema, Yesu alisema, “Wengi watakuja Kwangu na kusema, ‘Bwana, je, sikutoa pepo kwa Jina Lako? Na si mimi niliyefanya *hivi*? Na si mimi nimefanya *vile,* na mambo haya yote?’” Alisema, “Sikujua hilo. Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu.” Unaona?

Naamini wakati unakuja . . .

224 “Madhihirisho ya karama yalitolewa kwa kila mtu kwa faida yake.” Hiyo ni—hiyo ni kweli. Ninaamini karama ni nzuri, na tunazihitaji na kuziheshimu.

225 Lakini naamini wakati unakuja ambapo itakuwa katika kiwango cha juu zaidi ya hapo. Mbona, “Baada ya mambo haya yote kuondolewa, upendo utadumu milele.” Unaona? Ni upendo wa Mungu. Tutaninii tu—tutakuwa tu tumesimama, tukihubiri hivi, ama kuzungumza, na upendo tu utatua juu ya jengo hilo. Whiu! Jamani!

226 Unaona, hii ndiyo siku ya kuhubiri. Hii ndiyo siku tunayopaswa kuingia ndani na kuwachukua wenye dhambi na kuwatoa nje. Mnaona ninachomaanisha? Hiyo ndiyo mahubiri ya Neno yanayopaswa kufanya, ni kwa wenye dhambi, na kuwatoa. Sasa inabidi tuangalie, mle ndani, na sisi . . . Ishara na maajabu hufanyika kwa kuwekewa mikono, na kadhalika, kwa sababu ni kuhubiri.

227 Lakini ninaamini wakati unakuja sasa ambapo yeye karibu tu . . . Kanisa linakaribia kutia nanga. Unaona?

228 Mungu hatakuwa na mwili wa ajabuajabu. Hatakuwa na vidole sita kwa mkono mmoja. Kutakuwa na vidole vitano tu kwa mkono mmoja. Mwili wa Kristo hautakuwa wa ajabuajabu. Na wakati mtu wa mwisho ameingia katika Mwili wa Kristo, basi imekwisha. Imekwisha. Sijui ni ipi. Huenda hili limekuwa ndilo la mwisho, asubuhi ya leo. Huenda wewe umekuwa wa mwisho. Labda huko Afrika, leo, wa mwisho ataletwa. Lakini wa mwisho atakapokamilika, ninamaanisha . . . Unaweza kuendelea, kuhubiri Injili, lakini hakutakuwa na jibu. Unaona, hakuna jibu.

229 Nikizungumza na Billy Graham na wao, ambapo walikwenda mahali ambapo elfu thelathini, au ishirini au thelathini elfu waliongoka. Hawakuweza kupata watu ishirini au thelathini, ndani ya mwaka mmoja. Wazia jambo hilo, wazia tu jambo hilo. Unaona?

230 Sasa, hilo linanifanya kuwa Mkalvini, hasa. Unaona? Ambacho Mungu amefanya, Mungu amekifanya.

231 Sasa, Yesu hakuja duniani kusema tu, “Nitawafanya wahubiri waende na kuhubiri baadhi, wawaambie juu ya kile nilichofanya, na labda mtu atanihurumia na kuokolewa.” Mungu haendeshi ofisi Yake namna hiyo.

232 Hapo, Mungu, hapo mwanzo, alijua ni nani hasa angeokolewa. Yesu alikuja kuokoa wale ambao Mungu alijua wangeokolewa. Hakuwa tayari kwamba wangepotea, bali, akiwa Mungu, alijua ni nani angepotea na ni nani angeokolewa. Kwa hiyo, Yeye angeweza kukusudia tangu awali. Si kukusudiwa tangu awali, Yeye—Yeye kimbele-. . . Kwa kujua kimbele, Angeweza kuweka katika utaratibu, kufanya kila kitu kifanye kazi kwa utukufu Wake. Kwa sababu, hiyo . . .

233 Ibilisi—ibilisi hayupo kila mahali wala si mweza yote, wala hajui mwisho tangu mwanzo. Mungu pekee ndiye anajua. Hilo ni jambo moja, Mungu yuko tu *Hapa* juu. Anajua. Ibilisi hajui kitakachotokea. Hajui kitakachotokea. Jambo pekee analojua, yeye ni ibilisi tu, na anafanya tu anachoweza kufanya. Na kila kitu anachoweza kuingia, anakifanya.

234 Lakini, Mungu anajua mwisho. Amina. Kwa hivyo, Mungu akijua mwisho, anaweza kufanya kila kitu kifanye kazi kwa utukufu Wake. Amina. Loo, ninampenda. Jamani, loo, jamani! Unaona? Yeye ni Mungu. Kwa hiyo, kumbukeni, wakati mtu wa mwisho aliyekuwa na ninii yao . . .

235 Ni lini jina lako liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo; jana, mwaka jana, mwaka kabla ya mwaka jana? Hapana, bwana. "Wakati ulimwengu ulipoumbwa, jina lako liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo," kile ambacho Biblia ilisema. Biblia ilisema, katika Ufunuo, "Na mpinga-Kristo akawadanganya wote wakaao juu ya uso wa nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Jina lako liliandikwa wakati huo. Sasa, jambo pekee . . .

Unasema, "Ni nini kuhubiri Injili, basi?"

236 Vema, Biblia inaeleza jambo hilo waziwazi. Unaona? Alisema, "Ufalme wa Mbinguni unafanana na mtu aliyechukua wavu akaenda baharini au ziwani. Naye akatupa wavu baharini, naye akauvuta." Huko ni kuhubiri Injili. Unaona? Kuna bahari nzima. Marekani ni ziwa. Nao wahudumu . . .

237 Sasa, ninashuka hapa, nasimama Jeffersonville, kwenye kona *hii* ya ziwa. Nasema, "Ndugu Neville, umekuwa ukivuta juya?"

"Naam."

"Unapata chochote?"

"Si sana."

238 "Vema, hebu . . . Nitavuta pamoja nawe kwa muda kidogo." Nami nitatupa wavu wangu huko, naye anatupa wake. Na hapa tunavuta, kuhubiri, kuvuta ndani.

239 Kundi la watu wanakuja, wanasema, "Naam, ninataka kumpokea Bwana Yesu." Vema.

Angalia pande zote, "Samaki ni yupi? Yupi?"

"Sijui." Unaona?

"Vema, sasa, utafanya nini sasa?"

240 "Vema, ninaenda California. Bwana alinituma kule California. Ninaenda kuvua huko kwa muda."

241 Nitaenda kule na kutupa wavu wangu namna *hii*, na kusukuma ndani, elfu moja mia tano wanakuja kwa wakati mmoja. "Je, wote waliokolewa?" Sijui. Hao hapo. Ninachukua wavu. Huo ndio wavu wa Injili.

242 Baadhi yao, Biblia ilisema, pamoja na kila namna ya vitu vilivyokuwa majini. Wote walipumua juu ya maji yale yale, wakaishi katika maji yale yale. Hiyo ni kweli? Unaona? Kulikuwa na kasa wa maji safi, kasa wa matopeni, nyoka, vyura, mijusi, wala mizoga, na samaki halisi.

243 Sasa, wale waliokuwa samaki wakati wavu wa Injili ulipowashika, walikuwa ni samaki walipokuwa ukingoni. Wale ambao walikuwa kasa katika wavu wa Injili, walikuwa kasa kwenye ukingo. Haitachukua muda mrefu mpaka watakapoyarudia matope moja kwa moja tena. "Kama nguruwe kwenye kugaagaa kwake, na mbwa kwenye matapishi yake," wanatoweka. Unaona?

244 Lakini, hapo mwanzo, walikuwa kasa, kwanza kabisa. Si kazi yangu kusema wao ni kasa. Sijui. Ninavuta tu juya, unaona, navuta tu wavu. Lakini wakati samaki wa mwisho ametoka majini, ndugu, hakuna lingine.

Loo, Bwana Mwenyewe atakuja
Na atasema kazi imekamilika,
Kituo kitabadilishwa baada ya muda.

245 Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Atasema, "Kazi imefanywa, na imekamilika. Yote yamekwisha," wakati wa mwisho ametoka.

246 Na kumekuwa na maskini kundi la nguruwe wanaogaagaa huku, na kila kitu. Mungu anawatoa hao samaki kutoka pale, upesi tu awezavyo. Wahubiri kutoka kila upande, wakizungusha tu nyavu kutoka upande mmoja hadi mwingine. Hata tunafungana nyavu sisi kwa sisi. Tunavuta kwa bidii tuwezavyo, tukivuta juya. Yuko karibu tu kuwa tayari. Atalipua dimbwi hilo la kale, moja ya siku hizi, naye atakuwa amekamilika kabisa. Lakini samaki watakwenda kwenye maji mazuri, safi, huko nje, ambako watakuwa na Uzima wa Milele bila kikomo. Amina. Loo, huyo wa mwisho atakapokuja! Jamani!

247 Vipi, ni fursa iliyoje, kwa Mungu kusema, "Je, ungependa kuwa samaki?" Amina. "Je, ungependa kuwa samaki kwenye meza Yangu? Je, ungependa kuja na kuwa nyama kwenye meza Yangu?" Loo, jamani!

"Hakika. Hakika, Bwana." Unaona? Lakini asili yao ni samaki. Unaona?

248 Unapokuwa Mkristo, asili yako ni Mkristo. Sio lazima useme, "Sasa hu—hu—huwezi, huwezi kuvuta sigara. Huwezi kunywa pombe. Huwezi kuifanya." Sio lazima useme hivyo. Hawafanyi tu, kwa vyovyote vile. Unaona? Asili yao ni tofauti. Roho wa Kristo yuko ndani ya mtu huyo, na Kristo hafanyi mambo hayo. Unaona?

249 Unasema, "Unapaswa kumpenda Bwana. Unapaswa kwenda kanisani." Huna haja kuwaambia watu hao hivyo. Wanaenda, kwa vyovyote vile. Watapita kwenye mvua. Watakwenda. Wanapitia kifo, kwenda kanisani. Hakika. Wanaipenda. Inawabidi tu kufika huko. Ni hayo tu. Ni maisha yao. Wasipoenda, wa—wanahisi kana kwamba wanaangamia. Hakika. Naam, bwana. Huna budi kufika tu pale, na wakati wowote kitu fulani kinawaka moyoni mwako. Sio kwenda huko kubishana, sasa, sio kwenda huko kugombana, lakini kwenda huko kuabudu. Jamani! Na unaenda nyumbani ukiwa umeburudishwa. Je, hayo si ni maisha ya ajabu? Ni wangapi wamepitia hayo? Hebu tuone mkono wako. Loo!

250 Hiyo ni kweli, Gertie. Hebu tuimbe huo. "Amani! Amani!"

> . . . Amani! Amani ya ajabu,
> Inayoshuka kutoka kwa Baba huko Juu;
> Iloweshe roho yangu milele, naomba,
> Katika mawimbi yasiyopimika ya upendo.

251 Nataka ufanye jambo fulani sasa. Yeyote anayeketi karibu na wewe, peana mikono nao, useme, "Mungu akubariki, ndugu, dada. Nataka kukutana nawe Mbinguni."

> Amani! Amani! amani ya ajabu,
> Inayoshuka chini kutoka kwa Baba huko Juu;
> Iloweshe roho yangu milele . . . (Loo, jamani!)
> Katika mawimbi yasiyopimika ya upendo.
>
> Chini msalabani ambapo Mwokozi wangu alikufa,
> Huko chini ambapo nililia nipate kutakaswa na dhambi;
> Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
> Utukufu kwa Jina Lake!
>
> Utukufu kwa Jina Lake!
> Utukufu kwa Jina Lake lisilo na kifani!
> Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
> Utukufu kwa Jina Lake!

252 Sasa tunapoimba kifungu kifuatacho, sijui kama wagonjwa wangeweza kupanga mstari, papa hapa sasa, kwa ajili ya maombi, moja kwa moja upande *huu*. Nami ninataka wahudumu, kama watajitokeza sasa kutusaidia kuwaombea

wagonjwa. Pangeni mstari upande wa kulia, zungukeni *huku*. Hiyo ni kweli, upande wa kuume, wale wa kuombewa.

Nimeokolewa kutoka dhambini kiajabu sana,
Yesu anakaa ndani kwa utamu sana,
Pale msalabani ambapo alinichukua;
Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu kwa jina Lake la thamani!
Utukufu kwa jina Lake la thamani!
Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

253 Tupe sauti ya *Tabibu Mkuu*, tafadhali, Dada Gertie, ukiweza.

254 Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. (Nitapata hizo. Ndiyo, bwana.) Hivi mnakuja mkiwa na matarajio, ama kwa matarajio, hasa, kwamba mtaponywa asubuhi ya leo? Je, hilo ndilo lililo moyoni mwako, ndani kabisa? Kama unakuja hivyo, rafiki yangu, nitakuhakikishia tu ya kwamba uponyaji wako ni hakika tu kama wokovu wako, hakika kabisa.

255 Sasa, uponyaji wako si wa kudumu kama wokovu wako. Uponyaji wako utashindwa. Unaweza kuwa. . .Ikiwa umeponywa, utakuwa mgonjwa tena. Unaweza kuponywa leo, ukiwa na nimonia, mzima kabisa na mwenye afya, umetangazwa "mzima," na daktari, na wiki ijayo ufe kwa nimonia. Hiyo ni kweli.

256 Unaweza kuwa huna TB kabisa, wiki hii; na miezi miwili kutoka sasa, ufe, kwa kifua kikuu. Wangeweza kupitisha uchunguzi, bila hata chembe moja katika mwili wako, wanayoweza kupata; na kisha ufe katika wiki mbili zaidi, kwa kifua kikuu. Hiyo ni kweli. Unaona? Na huna budi kufa, hata hivyo.

257 Lakini, faida! Daudi alilia, "Msisahau faida Zake zote. Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana: na vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi Jina Lake takatifu. Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, wala usizisahau fadhili Zake zote." Faida! Je, ni nini faida katika safari? "Anayenisamehe maovu yangu yote." *Uovu,* ni jambo ambalo unatoka na kulifanya, na unajua hukupaswa kulifanya. Analisamehe. Unamwomba, Yeye anakusamehe. "Anayenisamehe maovu yangu yote; aniponyaye magonjwa yangu yote."

Sasa nataka kuwatatulieni hili, milele.

258 Kisha mtu anasema, "Ndugu Branham, unaamini katika uponyaji wa Kiungu?"

259 Sasa hebu niseme hili kwa busara na akili timamu. Nataka mtu fulani, daktari fulani, sayansi fulani, mahali fulani, ninawaalika katika uamsho huu, waje kwenye mimbara hii na kunionyesha mahali pamoja ambapo mtu yeyote aliwahi

kuponywa nje ya uponyaji wa Kiungu. Na—nataka uende kwa daktari wako, au kwa mtu yeyote unayetaka, na unionyeshe mtu yeyote aliyewahi kuponywa nje ya uponyaji wa Kiungu.

260 Nataka uniletee dawa ambayo itaponya. Nataka uniletee daktari anayesema kwamba yeye ni mponyaji. Atakuwa mtu wa kisigino, sawa, "kisigino," kisigino cha daktari. Bali Mungu Ndiye pekee awezaye kuponya, ama aliyepata kuponya, ama atakayewahi kuponya.

261 Kama tungekuwa na dawa ambayo ingeponya, tungeweza kumjenga mtu papa hapa kwenye jukwaa hili, tukiwa na dawa hiyo. Hiyo ni kweli, tungeweza kumjenga mtu, kumuumba papa hapa jukwaani.

262 Hebu wazia jambo hilo, uponyaji wote ni uponyaji wa Kiungu. Mungu anazo mbinu za kufanya hivyo.

263 Sasa unasema, "Vema, Ndugu Branham, nilifanyiwa upasuaji, uvimbe, ama kidole tumbo. Ikiwa daktari hangekuwa amekikata na kukitoa, ningekufa."

264 Hiyo inaweza kuwa. Huo pengine ni ukweli. Lakini ulijua daktari hakukuponya kamwe? Daktari aliondoa kizuizi. Alikata tu na kuondoa kidole tumbo. Hicho ndicho kitu kilichokuwa kinakuumiza. Lakini kamwe hakukiponya.

265 Umevunjika mkono. Unasema, "Vema, nilivunja. . . Ninaweka dau, ukivunja mkono wako, utaenda kwa daktari." Hakika ningeenda. Lakini hawezi kuuponya.

266 Vipi kama nikiingia ndani, niseme, "Daktari, niponye mkono wangu, upesi sana. Sina budi kulifanyia kazi gari langu alasiri ya leo"? Unaona? Mbona, ange—angejua ninahitaji uponyaji wa akili.

267 Angesema, "Naweza kuweka mkono wako." Lakini ni nani anayefanya uponyaji?

268 Unasema, "Ndugu Branham, vipi kuhusu penisilini, wanapokupa kwa ajili ya—ya ugonjwa, vijidudu katika mwili wako, kama zinaa na—na chochote ulicho nacho, nimonia? Hivi penisilini . . . Hivi penisilini haikuponyi?" Hapana, bwana.

269 Penisilini, penisilini ni kiua vijasumu, na kiua vijasumu ni muuaji. Kiua vijasumu huua. Dawa zingine zote huua. Dawa haijengi; huua. Dawa ni muuaji, si mponyaji. Nionyeshe dawa inayoponya. Nionyeshe dawa ambayo si muuaji, na huna dawa. Dawa huua, inaua vijidudu.

270 Kama vile tu ukiwa na panya nyumbani kwako, na uweke sumu ya panya. Na panya walikuwa wakila mashimo kupitia nyumba yako. Vema, sumu ya panya inaua panya, lakini haizibi nyumba yako. Unaona? Penisilini, penisilini huua kijidudu, lakini Mungu hana budi kuponya mahali ambapo kijidudu kimekula. Unaona ninachomaanisha?

271 Hata hivyo, Neno la Mungu, tutaingia katika hilo. Neno la Mungu haliwezi kujipinga Lenyewe. Ni Ukweli mtupu. Ni . . . Ninataka tu mtu huyo uje uweke kidole chako kwenye Neno, wakati wowote wakati wa uamsho, kunionyesha ukinzani katika Neno la Mungu, ambapo lilijipinga, haliwezi kunyooshwa na Neno la Mungu. Haipo. Hakika. Haipo. Hakuna ukinzani katika Neno, hata kidogo. Kabisa.

272 Unapata somo. Ninaweza kukuandikia barua moja na kukuambia jambo. Nikuandikie barua nyingine na barua nyingine. Jambo la kwanza unajua, hizi mbili zilikuwa zinaongea juu ya mada mbili tofauti. Unaona? Hakika.

273 Lakini Mungu Ndiye pekee aliyewahi kuponya, ambaye ataponya, ama angeweza kuponya. Ukivunja mkono wako, sasa, ningesema . . .

"Vema, nina uvimbe, vipi kuhusu hilo?" Sawa.

274 Sasa, kama mahali hapo padogo ambapo uvimbe huo umeshikiliwa, kama Mungu, kwa kuutoa ule uovu, na uhai ukitoka kwenye uvimbe huo, utakufa.

275 Ikiwa daktari ataukata, basi Mungu hana budi kuponya mahali ambapo daktari aliukata. Usipofanya hivyo, unatokwa damu hadi kufa. Je, hiyo ni kweli? Vipi kama akiondoa kidole tumbo kutoka kwako, na Mungu asikuponye, basi vipi kuhusu jambo hilo? Utakufa papo hapo.

276 Ukiziba moja ya mishipa mikuu katika barabara hii hapa nje. Wewe toka hapa nje na kuziba moja ya mishipa mikuu, na uone, kwenye mtaa huu hapa nje, mfereji huu wa maji machafu, na uangalie kinachotukia.

277 Hebu toka hapa nje na uzibe njia kuu, ukate vali kuu ya maji hapa chini, moja ya vali za maji, angalia kitakachofanya. Itailipua, hapa chini kwenye mfumo wa kusukuma maji.

278 Hakuna mahali, hakuna kitu, mfumo katika ulimwengu, kama mwili wa mwanadamu. Lakini unaweza kukata ateri vipande viwili, na kuibana hapa, na Mungu atafanya njia ya kupitisha hiyo damu na kuiingiza kwenye hiyo ateri tena. Ikiwa haikuwa hivyo; katika muda wa dakika moja, kama hiyo ikirudi nyuma na kugonga moyo wako, wewe, [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] ungekuwa umekufa, namna *hiyo*, mara ya kwanza unapojikuna.

279 Ni nani mponyaji? Loo, jamani! Mungu ndiye mponyaji. Unaona, huwezi kuwa na mifumo ya kimitambo inayofanya kazi hivyo. Lazima iwe isiyo ya kawaida.

280 Nilidungwa kwenye ateri mbili, katika miguu yangu yote miwili. Unaona? Na Mungu . . . hapo, mimi, maskini mvulana mdogo mwenye dhambi, nikifa kwenye uwanja huo. Mungu alijua alitaka nihubiri Injili. Yeye akapitisha damu. Sijui hata

habari zake, isipokuwa mtu aniambie, au nikitazama chini na kuona kovu. Unaona? Mungu, katika ateri!

281 Ukivunja ukanda mkuu kwenye hii, pampu hapa kwenye mfumo huu wa kusukuma maji, angalia hapa serikalini, nini kinatokea. Itarudi pale na kuilipua. Hakika, italipua. Hayo maji yanasukuma kwa nguvu namna hiyo, yatarudi nyuma moja kwa moja.

282 Lakini Mungu hufanya njia ya kukwepa na kuzunguka. Ni nani anayefanya hivyo? Ni akili gani hufanya hivyo? Nionyeshe mfumo wa maji utakaofanya hivyo. Haleluya! Ni akili ya Mungu. Ni Muumba mkuu anayefanya hivyo. Ndiyo, kwa kweli.

283 Ni nini hufanya mti kuwa tofauti na mwingine? Ni nini hufanya rangi ya ndege mmoja na mwingine, tofauti? Ni nini hufanya hotuba yake kuwa tofauti? Ni nini kinatufanya tuwe vile tulivyo? Ni Akili fulani. Ni Mungu.

284 Usiogope sasa. Alifanya-. . .Hii ni ahadi Yake. Si Ndugu Branham. Ni ahadi Yake. "Mimi ndimi Bwana niponyaye magonjwa yako yote." "Mtu akiwa mgonjwa, waite wazee wa kanisa, wapakeni mafuta, waombee, maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa huyo. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Na basi wakati agizo hilo limefanywa, likubali vile vile tu kama vile ungetubu na kubatizwa hapa. Tembea mara moja, useme, "Ni kazi iliyomalizika. Yote yamekwisha." Unaona?

285 Lakini tunatazamia mwujiza fulani mkuu kutokea. Hutokea wakati kuna imani ya kutosha kuufanya utokee. Lakini kama hakuna imani ya kutosha kuufanya utokee, utatukia hata hivyo, baada ya muda.

286 Angalia kile Yesu alisema katika tafsiri pale, aliposema kuhusu mlima. Alisema, "Baada ya muda, yatatimia. Ukiuambia mlima huu usogee, na uamini moyoni mwako utasogea," kasema, "baada ya muda, itatimia." Unaona? Itatimia.

Sasa wewe ni mgonjwa. Wengi wenu mnakufa, katika hali mbaya.

287 Naona wamemshika mwanaume fulani hapa sasa. Mtu mgonjwa sana. Kansa ni kitu cha kutisha, lakini Mungu anaweza kuponya kansa. Jamani! Naweza kukuonyesha hapa ndani. Ni wangapi hapa ndani wamewahi. . .Je, kuna mtu yeyote hapa sasa, ambaye amewahi kuponywa kansa? Inua mikono yako. Angalia hapa, ni kote kanisani. Unaona? Hakika, kila mahali. Tumekuwa nao wakiletwa, maana Mungu ndiye mponyaji.

288 Sasa, kila mmoja wenu huko nje, kwa kushukuru, ninawatakeni mwinamishe vichwa vyenu, nataka mwombe. Ndugu Neville, njoo hapa. Na sasa kama ninyi watu. . .Nataka wazee waje hapa, ili tuwaombee hawa watu. Na unapokuja hapa. . .Fanya hivi sasa. Unapokuja hapa, amini kwa moyo wako

wote. Na uchukue tu ninii langu. . . si neno langu, bali Neno la Mungu, kwa ajili yake. Amini tu kwa moyo wako wote. Hilo linatosha. Hilo ndilo. Yote yamekwisha. Mungu alisema hivyo. Neno Lake lilisema hivyo. Haliwezi kushindwa.

289 "Sijali jinsi ninavyohisi. Ninaendelea moja kwa moja, kwa vyovyote vile, nikisema ni Kweli." Angalia kinachotokea.

290 Lakini, unaona, kama tukisimama nyuma na, kusema, tuje kwa mstari wa maombi namna *hii*, kamwe haitokei. Ni hayo tu.

*MUNGU HUTIMIZA NENO LAKE* SWA57-0407M
(God Keeps His Word)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 7 Aprili, 1957, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org